# Nipashe

Jumatatu Novemba 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581857

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




UKURASA WA 3

**Basi** lagonga treni ya mizigo, mabehewa yaanguka



UKURASA WA 3

**Ahukumiwa** kifungo cha maisha gerezani kwa kusafirisha bangi

UKURASA WA 10

**Wahitimu** wa TASAF wagoma kuondolewa kwenye ruzuku

UCHAGUZI WA MITAA

# Upinzani walia wagombea wao wengine kuenguliwa

• **CHADEMA**, ACT, CUF wang'aka; Majaliwa atoa neno kwa viongozi wa vyama vya siasa... *Uk. 2&5*




Rahma Mwita



John Mrema

# 161,000 'wakacha' mtihani wa kidato IV ukianza leo

UKURASA 2





## BoT: Tunawatambua wakopeshaji wanne tu mikopo ya mitandaoni

UK. 4





Skani hapa kutembelea chaneli yetu


MICHEZO VIPIGO VITANO VIKALI KWA YANGA LIGI KUU UK.14 MAONI, UK.6

# 161,020 'wakacha' mtihani kidato cha nne ukianza leo

**Na Romana Mallya**

MTIHANI wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) 2024 unaanza leo, lakini wanafunzi 161,020 sawa na asilimia 23.3 waliopaswa kuufanya, hawatakuwa miongoni mwa watahiniwa.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitangaza kuanza kwa mtihani huo utakaofanyika kuanzia leo hadi Novemba 29, mwaka huu.

"Mwaka juzi wakati wanafunzi hao wanafanya Mtihani wa Kidato cha Pili walikuwa 690,341, lakini walioandikishwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne 2024 ni 529,321.

"Kuna upungufu wa takribani wanafunzi 161,000 waliofanya mtihani kidato cha pili ambao walitakiwa kufanya mtihani huu wa kidato cha nne na hawapo katika orodha ya waliosajiliwa mwaka huu," alisema.

Dk. Mohamed alisema ili kujua mahali walipo wanafunzi hao, ni suala la kujiridhisha kimkoa, halmashauri na katika ngazi ya kata kwa kila shule waliofanya Mtihani wa Upimaji Kidato cha Pili walikuwa wangapi na sasa waliofanya mtihani huu wako wangapi.Akizungumzia mtihani huo wa kidato cha nne mwaka huu, Katibu Mtendaji huyo alisema jumla ya watahiniwa 557,731 wamesajiliwa kuufanya. Kati yao, watahiniwa wa shule ni 529,321 na wa kujitegemea ni 28,410.

Alisema kuwa kati ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa mwaka huu, wavulana ni 250,562 sawa na asilimia 47.34 na wasichana ni 278,759 sawa na asilimia 52.66.

Dk. Mohamed alisema kuna watahiniwa wa shule 1,088 wenye mahitaji maalumu. Kati yao, wenye uoni hafifu ni 601, wasioona ni 56, wenye uziwi ni 209, wenye ulemavu wa akili ni 39 na wenye ulemavu wa viungo ni 183.

"Kati ya watahiniwa wa kujitegemea 28,410 waliosajiliwa, wavulana ni 11,167 sawa na asilimia 39.31 na wasichana ni 17,243 sawa na asilimia 60.69," alisema.

Dk. Mohamed alisema wapo watahiniwa wa kujitegemea wenye mahitaji maalumu 18. Kati yao, wenye uoni hafifu ni mmoja, wasioona ni 16 na mmoja mwenye ulemavu wa viungo.

Alisema mtihani huo utafanyika katika jumla ya shule za sekondari 5,585 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 961.

Alisema maandalizi yote yamekamilika ikiwa ni pamoja na usambazaji mtihani, vijitabu vya kujibia na nyaraka zote muhimu zinazohusu mtihani katika mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Katibu Mtendaji huyo alisisitiza suala la usalama wa vituo vya mitihani na kutoa wito kwa wasimamizi walioteuliwa kuisimamia kwa kufanya kazi zao kwa umakini, uadilifu na kwa kuzingatia weledi na kanuni na miongozo waliyopewa ili kila mtahiniwa apate haki yake.

Aliwataka wasimamizi kuhakikisha watahiniwa wenye mahitaji maalumu wanaifanya ipasavyo, ili wapate haki yao ya msingi, ikiwamo kuwapa mitihani yenye maandishi yaliyokuzwa kwa wenye uoni hafifu.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalumu waongezewe muda wa dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika 10 kwa kila saa kwa masomo mengine kama mwongozo wa baraza unavyoelekeza," alisema.

Kwa upande wa watahiniwa, Dk. Mohamed alisema baraza linaamini wamejiandaa vizuri, hivyo halitaraji mtahiniwa yeyote kujihusisha na vitendo vya udanganyifu, kwa kuwa atakayebainika, matokeo yake yatafutwa kwa mujibu wa kanuni za mitihani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
08/11/2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 09-11-2024** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MASAKI AREA,** gari hilo lenye namba za usajili: T 176 DFN / T 171 DFN.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi MASAKI AREA kupitia BAGAMOYO ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***




Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Possi, akipokea zawadi ya taarifa za kesi kutoka kwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Aboud, alipotembelea mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna inavyotekeleza majukumu yake, jijini Arusha. **PICHA: EAC**

# Vyama vyalia wagombea wao wengine kuenguliwa

**Na Elizabeth Zaya**

ZIKIWA zimebaki siku 16 watanzania kuchagua viongozi wao kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, baadhi ya vyama vimeendelea kulia kutokana na wagombea wao kuenguliwa.

Chama cha ACT-Wazalendo kimesema katika Jimbo la Rufiji, wagombea wao 382 wameenguliwa, wakijumuisha wa nafasi ya wenyeviti wa vijiji 28, vitongoji 90 na wajumbe 264.

Kukiwa na kilio hicho ACT - Wazalendo, vyama vingine vya upinzani vimedai kuwa wagombea wake wengi majina hayaonekani kwenye orodha ya walioteuliwa tangu Novemba 8, mwaka huu na kuanza mpango wa kukata rufani kutaka warejeshwe.

Viongozi wa vyama hivyo wamedai kuwa wakiwa katika harakati za kukata rufani, hata wachache walioteuliwa siku hiyo, nao jana walianza kuenguliwa.

Miongoni mwa vyama ambavyo vimeendelea kulia kukumbwa na kadhia hiyo mbali na ACT, ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama cha Wananchi (CUF).

CHADEMA imesema kuwa ikiwa inapambana kushughulikia rufani kwa wagombea wake ambao majina yao hayakuonekana siku ya kwanza baada ya orodha ya walioteuliwa kutoka, limeibuka lingine kwa wagombea waliokuwa wameteuliwa nao kuanza kuenguliwa.

"Tulikuwa bado tunashughulikia suala la kukata rufani na mpaka sasa ni baadhi tu ya maeneo ambayo rufani zetu zimepokewa ila maeneo mengi walifunga ofisi na kutokomea," alidai Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema.

Katika mazungumzo na Nipashe jana, Mrema aliendelea kusema, "Wakati tunapambana kushughulikia hao walioenguliwa juzi (Novemba 8), tumepata taarifa nyingine kwamba bado watu wetu waliokuwa wameteuliwa awali nao wanaendelea kuenguliwa muda huu. Mfano, Manispaa ya Iringa, walioteuliwa wote, wameenguliwa.

"Tarime Vijijini, Sumbawanga, Same, Buhigwe, Manonga, Igunga, Rufiji, Tunduma na maeneo mengi ya nchi, bado watu wetu wanaenguliwa, hivyo tunaendelea na hatua ya kukata rufani japo hatujui kama tutawakuta wahusika ofisini ili wapokee rufani zetu au watafunga, tutajua idadi yote kamili baadaye baada ya kazi ya kuengua itakapokamilika," alisema Mrema.

Alisema sababu kuu ambayo wameambiwa wagombea wao wanaenguliwa ni kutokana na kuwekewa pingamizi.

"Kwa mfano, Iringa wagombea wetu wameambiwa wamewekewa pingamizi ila hawajapewa nakala kama ulivyo utaratibu ili wajibu hayo mapingamizi. Maeneo mengine wanapigiwa simu kuambiwa wameenguliwa," alisema Mrema.

Msemaji wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Chama cha ACT-Wazalendo, Rahma Mwita, naye alilalama wagombea wengi wa chama hicho waliokuwa wamepitishwa, nao kuenguliwa kwa madai ya kuwekewa pingamizi, wakidaiwa kwamba hawajui kusoma na kuandika.

"Wale waliokuwa wameenguliwa ile siku ya kwanza Novemba 8, majina yalipotolewa, tulifanikiwa baadhi yao kukata rufani wakarejeshwa, lakini tatizo lingine limeibuka wameondolewa tena, eti wamewekewa pingamizi.

"Si wao tu hata maeneo mengi ambako wagombea wetu walipita, nao wameondolewa. Kwa mfano, maeneo ya Ruangwa, Lindi, Kibiti, Rufiji, Bariadi, wameondolewa wote," alisema Rahma.

Alisema chama hicho kinapanga kukaa kikao na kitatoa tamko la msimamo wa chama wakati wowote.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma wa CUF, Mohamed Ngulangwa, alisema ombi kubwa la chama hicho ni serikali iwarejeshe wagombea wote walioenguliwa.

"Sisi tumesema hili tangu jana (juzi) baada ya wagombea wetu wengi kuenguliwa. Lakini kubwa ni wito wetu kwa serikali, kwamba wagombea wote walioenguliwa kwa hila kwa vyama vyote vya upinzani, warejeshwe bila urasimu ili wananchi wakachague viongozi wanaowataka Novemba 27," alisema Ngulangwa.

Juzi baada ya kuwekwa hadharani majina ya walioteuliwa na wasioteuliwa kugombea nafasi za uenyekiti na ujumbe, baadhi ya vyama vilitoka hadharani na kudai wagombea wake 'kukatwa' huku vikionesha kutoridhishwa na sababu zilizotolewa.

Kwa mujibu wa kanuni 18 GN Na.571 na 574, ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (2024), uteuzi wa wagombea ulipaswa kufanywa Novemba 8, mwaka huu.

Pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea ni kuanzia Novemba 8 hadi 9 na uamuzi wa pingamizi ulipaswa kutolewa kuanzia Novemba 8 hadi 10 jana, hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 23.

Rufani dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi zitapokewa kuanzia Novemba 10 na 13 na uamuzi wa kamati ya rufani utatolewa kuanzia Novemba 10 hadi 13 mwaka huu, hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 23.

Kadhalika, kampeni za uchaguzi huo zitafanyika kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni kuanzia Novemba 20 hadi 26, kwa mujibu wa kanuni ya 26.

# Basi lagonga treni, mabehewa yaanguka

**Na Halfani Chusi**

ABIRIA 14 wamenusurika kifo katika ajali iliyohusisha basi na treni ya mizigo iliyotokea juzi katika makutano ya reli Malagarasi na Nguruka, mkoani Kigoma.

Kwa muujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Shirika la Reli Tanzania (TRC), treni ya mizigo yenye namba za usajili Y611 iliyokuwa ikitokea Kigoma kuelekea Tabora, iligongwa na basi lenye namba za usajili T 545 DJW, mali ya kampuni ya Clasic linalofanya safari zake Kigoma-Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilifafanua zaidi kuwa ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia juzi na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa basi kulipita basi lingine lililokuwa limesimama mbele kwa ajili ya kupisha treni, hivyo kugonga treni.

Ajali hiyo ilisababisha mabehewa matano kati ya 30 kuanguka na kusababisha majeraha kwa abiria wa basi ambao kati yao, wanane walikuwa wanawake na sita wanaume na hakuna aliyepoteza maisha.

Kupitia taarifa hiyo, TRC ilitoa wito kwa madereva na watumiaji wa barabara kufuata sheria na kuheshimu vivuko vya reli ili kuzuia ajali zinazoweza kuepukika.

# Matukio 1,800 ya wanyamapori yadhibitiwa

**Na Grace Gurisha**

MATUKIO 1,806 yamedhibitiwa Ukanda wa Ruvuma kupitia doria za udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika kipindi cha kuanzia 2023/24 hadi 2024/25 zinazofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Doria maalumu za udhibiti wa mifumo hifadhini ktika kipindi hicho zilikuwa na jumla ya mifugo 2,152 iliyokamatwa katika maeneo ya hifadhi kwenye ukanda huo na hatua za kisheria zilichukuliwa.

Hayo yalisemwa mwisho wa wiki jijini Dar es Salaam na Ofisa Wanyamapori Mkuu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Antonia Raphael wakati akiwaeleza waandishi wa habari mikakati ya serikali katika utekelezaji mradi wa kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika Ukanda wa Ruvuma. Alisema mradi huo ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani, waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) wakishiriki katika mradi huo.

Alisema mikakati ya serikali inajumuisha kuchimba mabwawa 30 katika Hifadhi za Taifa za Serengeti (5), Nyerere (2), Saadani (2), Mikumi (2), Tarangire (2) na Mkomazi (3) na Pori la Akiba la Selous.

"Hatua iliyofikiwa, mabwawa saba yamechimbwa Hifadhi ya Nyerere (1), Mkomazi (1), Tarangire (1), Mikumi (1) na Serengeti (2) na Pori la Akiba Swagaswaga (1)," alisema Raphael.

Mkurugenzi Msaidizi wa wizara hiyo, Dk. Fortunata Msofe, alisema jumla ya Sh. bilioni 45.1 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu mwaka 2024/25 nchi nzima.

Mwenyekiti wa JET, Dk. Ellen Otaru alisema waandishi wa habari wanatakiwa kuandika habari ambazo zitasaidia jamii na si sitakazowatisha, hasa katika suala la mgongano wa binadamu na wanyamapori kwa sababu imejikita katika wanyama.

"Habari zenu mziandike kwa stahili ya hadithi si za kuwatisha wananchi, utaona tembo kaua mtu, lakini kuna namna unaweza ukaandika ikawaondoa hofu," alisema Dk. Otaru.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akipanda mche wa mchikichi pembezoni mwa Bonde la Mto Mpiji wakati wa uzinduzi wa programu ya upandaji miche 5,000 ya zao hilo, Kata ya Mambwepande, Dar es Salaam juzi ili kudhibiti mmomonyoko wa ardhi. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmassy na wa pili kushoto ni Ofisa wa Maji Bonde la Wami/Ruvu Kidakio cha Pwani, Diana Kimbute. **PICHA: FRANK MONYO**

# Jela maisha kwa kusafirisha bangi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imemtia hatiani Joshua Kiloso na kumhukumu kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 275.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki katika masijala ndogo Arusha mbele ya Jaji Immaculate Banzi baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa Juni 6, 2023, katika kijiji cha Losinoni Juu, wilayani Arumeru, mkoa wa Arusha, mshtakiwa alikutwa anasafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 275.

Mshtakiwa alikana mashtaka na upande wa mashtaka kwa kuthibitisha makosa hayo, uliita mashahidi watano na vielelezo saba.

Katika shauri hilo, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Mseley Mfinanga aliyesaidiwa na Amanda Lushakuzi na upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Zuberi Ngawa.

Akisoma sehemu ya ushahidi, Jaji Banzi alisema shahidi wa pili alidai walipata taarifa mshtakiwa anajihusisha na biashara ya dawa za kulevya na walichukua hati ya kufanya upekuzi nyumbani kwake.

Inadaiwa walifanya upekuzi katika nyumba yake maeneo ya Losinoni Juu na kukuta viroba vikiwa na majani makavu yaliyosadikiwa kuwa dawa za kulevya pembeni mwa kitanda.

Shahidi alidai walikuta viroba 11 vyenye dawa hizo na mshtakiwa alipoulizwa, alikiri kwamba ulikuwa mzigo wake.

Inadaiwa shahidi wa tatu alichukua sampuli ya majani kwa ajili ya uchunguzi na baada ya uchunguzi taarifa kutoka kwa mkemia ilibainisha kuwa majani hayo yalikuwa bangi.

Mshtakiwa, wakati wa kujitetea, alikana kuhusika katika tukio hilo, alikana kukamatwa eneo la tukio, ambalo ni nyumbani kwake na pia alikana kuitwa Joshua Akwii Msila na kudai jina lake halisi ni Joshua Msila Kiloso.

Alidai kuwa Mei 27, 2023 alikuwa Ngaramtoni anauza viazi na maparachichi ndipo alipokamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi KIA, alikaa wiki tatu, akahamishiwa Polisi Boma akawekwa mahabusu siku mbili na kuhamishiwa Kituo Kikuu cha Polisi Arusha ambako alikaa mahabusu hadi Juni 15, 2023 alipopelekwa mahakamani.

"Mahakama imezingatia ushahidi wa pande zote mbili. Hoja iliyopo ni endapo upande wa mashtaka wameweza kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote.

**"Mahakama imezingatia ushahidi wa pande zote mbili. Hoja iliyopo ni endapo upande wa mashtaka wameweza kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote.**

"Kwa mujibu wa kanuni, ni wajibu wa upande wa mashtaka kuthibitisha shtaka kwamba mtuhumiwa alisafirisha kilo 275.0 za bangi kama inavyodaiwa kwenye shtaka," alisema.

Jaji alisema kuna ushahidi wa moja kwa moja wa shahidi wa pili unaodai mshtakiwa alikamatwa nyumbani kwake, walifanya upekuzi na kukuta viroba 11 vya bangi na kwamba ushahidi huo unaungana na ushahidi wa mashahidi wengine walioshuhudia upekuzi.

"Kama mshtakiwa anadai hakukamatwa eneo la tukio, alitakiwa kusema hayo mapema wakati wa usikilizwaji wa awali, mshtakiwa alikana kuitwa Joshua Akwiina kudai huyo ni mtu mwingine.

"Hakuna ubishi kwamba jina hilo ni tofauti na Joshua Msila Kiloso na kisheria ni watu wawili tofauti," alisema Jaji Banzi. Alisema kwa mujibu wa shahidi wa pili ni kwamba mshtakiwa alijitambulisha mwenyewe jina hilo na alijitambulisha hivyo ili kukwepa kesi.

"Baada ya kupitia ushahidi, mahakama inaona upande wa mashtaka umeweza kuthibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa bila kuacha shaka, mshtakiwa alikutwa na bangi viroba 11 nyumbani kwake, hivyo mahakama inamtia hatiani kwa kosa alilloshtakiwa nalo la kusafirisha dawa za kulevya.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, mtuhumiwa akitiwa hatiani, adhabu ya lazima ni kifungo cha maisha. Katika kosa hilo sina chaguo lingine bali kumpa adhabu ya lazima, hivyo mahakama inamuhukumu kifungo cha maisha gerezani Joshua Msila Kiloso kwa jina maarufu Joshua Akwii Msila.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

MIKOPO MITANDAONI

# BoT: Tunawatambua wakopeshaji wanne tu

Na Mwandishi Wetu

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imekiri kuwapo kasoro kwenye shughuli za ukopeshaji mitandaoni, ikirejea kati ya maombi 16 iliyopokea, manne pekee ndiyo yamekidhi vigezo.

Sambamba na hilo, BoT imebaini ukiukwaji wa sheria kwa Watoa Huduma Ndogo za Fedha (Microfinances) kuanzisha 'aplikesheni' za kukopesha mtandaoni kinyume cha sheria walizowekewa.

Ni ufafanuzi uliotolewa na Meneja Msaidizi Idara ya Microfinance wa BoT, Mary Ngasa, alipozungumza na Nipashe ofisini kwake wiki iliyopita jijini Dar es Salaam kuhusu kuwapo ukiukwaji huo wa sheria, hata kudhalilisha wakopaji.

"Kati ya maombi ya aplikesheni 16 kwa ajili ya kutoa mikopo mtandaoni, manne pekee yamekidhi vigezo na kupewa leseni za kukopesha mtandaoni, huku aplikesheni 55 zilikabidhiwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ili waziondoe mtandaoni," alisema.

Mary alisema aplikesheni zilizopewa kibali, zinatakiwa kuweka wazi kuwa zinafanya kazi kwa mujibu wa leseni inayotolewa na BoT, kuweka wazi masharti ya mikopo na mawasiliano ambayo wateja wanaweza kuyatumia kuwasiliana nao kwa jambo lolote.

Alisema BoT pia imebaini aplikesheni hizo zina muunganiko na Microfinances ambazo zimetumia fursa ya kuwapo teknolojia, kuanzisha aplikesheni za kukopesha mtandaoni, na kwamba zipo microfinances zenye hadi aplikesheni 10 za kukopesha mtandaoni.

"BoT imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya Microfinances nne ambazo zilianzisha aplikesheni na kutoa mikopo mtandaoni bila kibali cha BoT kama leseni yao inavyowataka.

"Wanaotoa mikopo mtandaoni bila kibali, waliogundulika hadi sasa ni 55 na licha ya tangazo kuwataka wajisajili hawajafanya hivyo. Tulivyotoa mwongozo wa kuwataka walete maombi hawajaleta, lakini tumewafuatilia mtandaoni na kuwabaini," alisema.

Akifafanua zaidi, Ofisa Idara ya Microfinance, Deogratius Mnyamani alisema: "Tulianza uchunguzi wetu muda mrefu, tukabaini kuna zaidi ya aplikesheni 71, tukaona taratibu zao, baadhi tuliwaita tukazungumza nao, ndipo tukatoa mwongozo, huwezi kuutoa hewani, lazima uwe umejiridhisha na mambo mengi.

"Leseni ya Microfinance inaruhusu kuongeza bidhaa nyingine, lakini wengi wakati wanaomba hawakueleza kwamba watakuwa wanatoa mikopo mtandaoni, na tulipofuatilia zaidi, tukabaini kuna wenye Microfinance moja lakini wana aplikesheni 10.



Gavana BoT, Emmanuel Tutuba

"BoT tunaposimamia tunataka kufahamu taarifa za utendaji wake wa kila mara, lazima atuletee sera ya ukopeshaji ambayo tunaipitia ili kujua aina ya mikopo, kiwango cha mikopo, muda, riba, namna ya ufuatiliaji, urejeshaji na dhamana. Anapotaka kufanya mabadiliko yoyote lazima atuletee BoT ili tuone kama inafikia viwango na masharti yaliyowekwa."

Kaimu Meneja wa Microfinance, Dickson Gama alisema BoT ilijipa muda kuchunguza suala hilo na kupata uzoefu wa nchi zilizopitia changamoto kama hiyo ili kuwa na mwongozo, na kwamba usimamizi wa huduma ndogo za fedha uliletwa kwenye benki hiyo mwaka 2018.

"Tulikuwa na watoa huduma binafsi wengi, vilio vilikuwa vingi kwa watu kutapeliwa mali, ndipo uhitaji wa sheria ya kusimamia hii sekta uliibuka," alisema.

Kuhusu udhalilishaji wakopaji mtandaoni unaoshuhudiwa nchini hivi sasa, Gama alisema: "Utaratibu ni kwamba mtu amekopa, hajalipa unampa notisi ya siku 14, hajajibu anapewa ya siku saba na baada ya hapo unachukua hatua kwa utaratibu kwa kuchukua dhamana yake kwa njia ya kisheria, lakini wanapotishia watu, wanavunja sheria nyingine za nchi."

Alisema ufuatiliaji wa BoT utakuwa endelevu. Kila mtoa huduma atachunguzwa na akibainika kuvunja sheria, watamchukulia hatua kwa kushirikiana na TCRA.

"Kama nchi nadhani itafika wakati tutawatafuta hata 'Play Store' ili wasizipandishe hadi wapate kibali cha mamlaka. Kuna nchi Google hapandishi aplikesheni zake hadi ajiridhishe na mambo ya kisheria," alisema.

Alifafanua kuwa hivi sasa kila mwenye aplikesheni aliyesajiliwa na BoT, lazima aoneshe ni nani, kibali alichopewa, namba ya leseni ya BoT na mawasiliano, na kwamba siku zijazo wataboresha ili kuwa na namba maalumu ya utambuzi kama imesajiliwa au la.

"Mikopo ya mtandaoni imetokea kutokana na maendeleo ya teknolojia ili kuwezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi kokote aliko. Hata hivyo, kuna changamoto watu wanatukanwa na kudhalilishwa, ila tumechukua hatua madhubuti kudhibiti kwa sababu ni jukumu letu kuhakikisha sekta iko salama," alisema.

Ofisa huyo wa BoT alisema Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, inaelekeza taasisi kuwa na wafanyakazi au chombo cha kupokea malalamiko kutoka kwa wateja ili kunapokuwa na changamoto, wawe na mahali pa kutolea dukuduku na ikishindikana ndipo wanaweza kwenda BoT.

"BoT tunasajili taasisi, ikishasajiliwa inaruhusiwa kutoa huduma, walaji wakiona wametendwa kinyume kama vile udhalilishaji, kutukanwa, kunyanyaswa, kusambaza taarifa kwa mtu mwingine, wana haki ya kumshtaki kwa mujibu wa Sheria ya Taarifa Binafsi (2022). Ili huyu mkopeshaji atoe huduma, ni lazima ajisajili kwenye Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPC).

"BoT tumeona katika ufuatiliaji wetu, kuna watu walikwenda polisi wakashtaki na kupata haki kama inavyostahili kwa mtanzania yeyote ambaye atatukanwa au kusambaziwa taarifa zake kwa watu wengine kinyume cha ridhaa yake, ana haki ya kuwashtaki," alisema.

Meneja Msaidizi Idara ya Microfinance wa BoT, Mary Ngasa alisema kuwa baada ya mwongozo wa mikopo mtandaoni, walitoa taarifa ya namna ya kusajili na tangazo kwa umma liliwataka wakopeshaji wawasilishe maombi ili yapitiwe na kupewa kibali.

"Tulitoa muda wa siku 14 walete maombi, wapo walioleta tumeyachakata na wamepewa vibali. Tulitaka kufahamu wanaofanya hizo biashara, ambaye ataendelea bila kibali tutachukua hatua kwa kushirikiana na TCRA, kuwatoa kwenye mtandao," alisema.

Oktoba 21, 2024, Nipashe ilichapisha ripoti ikiangazia namna ukopeshaji mtandaoni ulivyogeuka kero, ikiwamo udhalilishaji wananchi.

Uchunguzi wa Nipashe pia ulibaini masharti ya mikopo hiyo yanafichwa, riba kubwa inayozidi asilimia 80, huku Mbunge wa Viti Maalumu akieleza kwamba, wanawake 68 katika mikoa minane nchi wamefariki dunia kutokana na udhalilishaji baada ya kukopa.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# RC anusa ufisadi ununuzi zana za kilimo

Na Thobias Mwanakatwe, ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amenusa ufisadi katika Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) Utemini, Halmashauri ya Wilaya ya Itigi katika ununuzi wa zana za kilimo, likiwamo trekta lililonunuliwa kwa Sh. milioni 65 na kuagiza ukaguzi wa hesabu ufanyike haraka.

Akizungumza jana na wananchi wa kata ya Itigi Mjini baada ya viongozi wa AMCOS hiyo kumlalamikia Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, alisema ukaguzi katika ushirika huo utafanyika ndani ya siku saba kubaini kama kuna ufujaji fedha uliofanyika na wahusika watachukuliwa hatua.

"Nitaandika barua kwa DC, atatuma timu ya wakaguzi, watakagua kompyuta (laptop), mashine na trekta iliyonunuliwa kama ni bei halisi, mimi simwonei yeyote, wote ni wangu. Mnipe muda wa siku saba ukaguzi ufanyike," alisema.

Halima alisema alisema mkoa utafanya mkutano na kuongea na viongozi wa AMCOS zote mkoani Singida ili wapewe elimu ya namna ya kuendesha ushirika.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu, vyama vya ushirika vinapaswa kufanya ununuzi wa kitu chochote baada ya kumshirikisha Ofisa Ushirika wa eneo husika na si chama kuchukua uamuzi kwenda kununua kitu chochote bila kumshirikisha.

Hatua ya Mkuu wa Mkoa wa Singida kutoa agizo la kufanyika ukaguzi katika AMCOS ya Utemini ilitokana na Mwenyekiti wa AMCOS hiyo, Geofrey Ighimbi kueleza kwamba waliamua kwenda kununua trekta bila kumshirikisha Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Daniel Sandewa kwa sababu amekuwa akiwapiga fedha kwa kuongeza bei kila wanapokwenda kununua vifaa vya ushirika.

"Mheshimiwa RC (Mkuu wa Mkoa), tunafahamu utaratibu lakini changamoto iliyopo ni Ofisa Ushirika tokea mwanzo alikuwa anatupiga katika ununuzi wa vifaa tulivyoomba, anaendelea kutupiga, tukaamua kujiengua kwake na aliposafiri kwenda Mwanza sisi tukafanya kikao tukaamua kununua trekta kwa Sh. milioni 65," alisema.

Ighimbi alisema Ofisa Ushirika huyo amekuwa 'akiwapiga' fedha kwenye ununuzi wa vifaa, mfano kompyuta mpakato (laptop) ambayo kihalisia inauzwa Sh. 300,000 lakini yeye aliwanunulia kwa Sh. milioni 1.2 na mashine ya kupepeta dengu aliwanunulia kwa Sh. milioni nne wakati bei halisi wanayojua sokoni ni Sh. milioni 1.5.

Ofisa Ushirika, Sandewa alipoulizwa na Nipashe wakati wa mkutano huo kuhusu tuhuma hizo, alisema si za kweli na kwamba amekuwa akipambana na viongozi wa AMCOS hiyo, mfano mashine ya kupepetea dengu walitaka kuuziwa kwa Sh. milioni 13, akakataa.

Alisema hata laptop waliyouziwa ni mbovu na kwamba trekta nayo wameinunua kwa Sh. milioni 81 na si milioni Sh. 65 kama walivyoeleza.

Mwanachama wa AMCOS ya Utemini, Elizabeth Ngowi, alisema viongozi wa ushirika hao wamekuwa hawatoi taarifa za mapato na matumizi ya fedha kwa wanachama na hata vifaa vilivyonunuliwa ikiwamo trekta wanachama hawakushirikishwa.

Naibu Katibu wa AMCOS, Amani Hamis, alisema si kweli kwamba wanachama hawashirikishwi katika ununuzi wa vifaa kwa kuwa hata katika ununuzi wa trekta kulifanyika kikao Oktoba 12, 2024 ambacho ndicho kilitoa uamuzi wa ununuzi wa trekta hilo.

## HABARI KITAIFA

UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

# Majaliwa awataka viongozi vyama vya siasa kukemea uvunjifu wa amani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa wito kwa viongozi wa vyama vya siasa vitakavyoshiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuwa vinara katika kulinda amani na kukemea viashiria vyote vya uvunjifu wa amani.

"Hamasisheni wanachama wenu kushiriki katika uchaguzi huo huku wakizingatia kudumisha amani iliyoko. Wananchi wote waliojiandikisha katika orodha ya wapigakura wa Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wajitokeze kwa wingi kupiga kura katika vituo vyao siku ya Jumatano tarehe 27 Novemba 2024. Siku hiyo itakuwa ya mapumziko maalumu kwa ajili ya uchaguzi huo," ameelekeza. Ni wito aliotoa jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano Mkuu na Kongamano la Umuhimu wa Amani kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, jijini Dar es Salaam.

"Mheshimiwa Rais Dk. Samia amewasihi Watanzania na viongozi wa dini kuendelea kuitangaza amani ndani na nje," Waziri Mkuu Majaliwa alisema.

Katika kongamano hilo, ambalo linaratibiwa na Jumuiya ya Waislamu wa Madhehebu ya Shia Tanzania, Majaliwa alitumia fursa hiyo kuwasisitiza viongozi hao kuhamasisha wanachama wao kushiriki katika uchaguzi huo huku wakizingatia suala la kudumisha amani kwa muhimu mkubwa.

Majaliwa alisisitiza kwamba kila mtanzania mwenye sifa ajitokeze kupiga kura ili kuwachagua viongozi ambao ni mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa mtaa, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa serikali za vijiji na kamati za mitaa.

"Ikumbukwe kuwa kupiga kura ni wajibu na haki ya kikatiba ya kila mtanzania," Majaliwa alisema katika kipindi ambacho kuna malalamiko ya vyama vya upinzani kutotendwa haki katika uteuzi wa wagombea katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri Mkuu aliongeza kuwa serikali inatambua, inaheshimu na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na madhehebu ya dini pamoja na taasisi zote, ambapo licha ya kutoa mafundisho ya kiroho, taasisi za dini zimekuwa zinaunga mkono jitihada mbalimbali za serikali katika kutoa huduma za kijamii kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Alhad Mussa Salum alipongeza Jumuiya ya Waislam wa Shia Tanzania kwa harakati zake za kuhakikisha amani na utulivu wa Tanzania unaendelea kukua.

"Mimi ni shuhuda mzuri wa harakati za Shia wanazofanya ili kuhakikisha amani na usalama wa Tanzania unaendelea kuimarika," alisema.

# Huduma za televisheni kidijitali zaimarika nchini

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mawasiliano iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeonesha mawimbi ya televisheni kidijitali kwa mfumo wa ardhini (DTT) yanafikia asilimia 58 ya watu.

Ripoti hiyo ya robo mwaka Julai hadi Septemba mwaka huu, inaonesha mawimbi yanafika asilimia 33 ya nchi nzima kijiografia kutoka asilimia 32 Juni mwaka huu.

Mfumo wa DTT ulianza kutumika Tanzania mwaka 2014 baada ya nchi kuanza kutumia mfumo wa utangazaji wa televisheni kidijitali.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, mfumo wa utangazaji wa satelaiti unaofupishwa DTH, umeenea kwa asilimia 100 miongoni mwa watu, pia nchi nzima kijiografia.

"Mawimbi ya utangazaji wa redio ya FM yameenea kwa asilimia 78 miongoni mwa watu Septemba kulinganisha na asilimia 75.52 Juni mwaka huu. Yameenea kijiografia kwa asilimia 56.5 kutoka 49.94 kipindi hicho," alisema.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa TCRA ilitoa leseni mpya 15 za maudhui ya utangazaji kati ya Julai na Septemba, ikiwamo moja ya huduma za redio kimkoa, tano za redio kiwilaya na mbili za kijamii.

TCRA pia ilitoa leseni tatu za televisheni ya kulipiwa kitaifa robo mwaka ya Julai-Septemba 2024.

"Leseni nyingine zilizotolewa ni moja ya redio mtandao, moja ya watayarishaji na wachakataji maudhui ya kutolewa mitandaoni na mbili za blogu za habari na matukio yanayotolewa kwenye tovuti," alisema.

Alisema kuwa hadi Septemba 2024, TCRA ilishatoa leseni za huduma mbalimbali za maudhui na idadi kwenye mabano kama ifuatavyo: redio (246) na televisheni zisizolipiwa (33), televisheni za waya (63).

Nyingine ni leseni za televisheni za kulipia (29), televisheni mtandao (210), redio mtandao (10), blogu za habari na matukio (66) na posta na usafirishaji vifurushi (146).

Dk. Bakari taarifa inaonesha kupanda na kushuka kwa idadi ya watu wanaonunua huduma za televisheni kwa waya.

"Waliongezeka kutoka 14,350 mwaka 2020 kufikia 19,739 mwaka 2021 na 22,295 mwaka uliofuata, kabla ya kushuka hadi 16,223 mwaka 2023. Taarifa inaelezea kushuka huku kuwa kunatokana na wateja kuhamia mifumo mingine ya utangazaji wa televisheni," alisema.

Aidha, alisema wateja 18,820 waliunganishwa Juni 2024 na kwamba idadi hii iliongezeka kwa asilimia mbili na kufikia 19,153 Septemba mwaka huu.

Kuhusu huduma za televisheni kwa waya zimeenea zaidi mikoa ya Kanda ya Ziwa; Shinyanga inaongoza, ikiwa na wateja 4,845 waliounganishwa, ikifuatiwa na Tabora yenye 2,118.

Mwanza kuna wateja 2,075 na Dar es Salaam 1,169, na kwamba mikoa yenye wateja wachache wa huduma za televisheni kwa waya ni Mbeya ambayo ina 64, Manyara (91) na Tanga (230).




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushindani huu Ligi Kuu Bara ukiendelea utaipaisha zaidi

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imeingia raundi ya 10, huku kila timu ikiwa tayari imeshaonja ladha ya kufungwa.

Kwa raundi za mwanzo tu kabla hata kufika nusu msimu, pia kuelekea kipindi cha dirisha dogo ligi imeanza kuwa na ushindani mkubwa kuliko msimu uliopita.

Sare ya mabao 2-2 kati ya Simba na Coastal Union Oktoba 4, mwaka huu, katika Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, ilianza kuonesha kuwapo kwa hali ya ushindani.

Ni mechi ambayo Simba ilikuwa inaongoza 2-0 hadi mapumziko, lakini kwa hali ya kushangaza Coastal walirudisha mabao yote kipindi cha pili.

Ushindi wa dakika za mwisho ambao Simba iliupata dhidi ya Mashujaa FC, Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, uliendelea kuonesha msimu huu si wa lelemama na timu zimejipanga.

Baada ya hapo tukashuhudia Mabingwa Watetezi, Yanga walipoteza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu, wakifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Jumamosi ya Novemba 2, Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam, kabla ya Alhamisi iliyopita kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United.

Hii inaonesha kuwa msimu huu timu zimejipanga kisawasawa kupambana kikwelikweli na kuondoa woga kwa timu kubwa.

Tulichoshuhudia ni kwamba msimu huu timu pamoja na kupaki basi zimekuwa zikipata muda wa kwenda kushambulia kwa kasi dhidi ya timu kubwa, ambazo mara nyingi huwa hazipo kwenye shepu nzuri zinapokuwa zinashambulia.

Tatizo ni kwamba timu nyingi zilikuwa na tabia ya woga na kutotumia nafasi zinapofanya mashambulizi ya kushtukiza.

Mpaka kufikia raundi hizi Ligi Kuu inaonekana imechangamka na kuvutia wengi. Hii sasa ndiyo inaweza kufanya mashabiki wakavutika kwenda viwanjani kwa sababu wanaona kuna upinzani. Mashabiki wa soka mara nyingi huwa hawapendi kutazama mpira ambao wanaona timu fulani ni lazima ishinde.

Mapokezi makubwa walioyapata Tabora United kila basi lao linapoonekana kuanzia Dar es Salaam hadi Tabora ni ishara tosha ya kwamba mashabiki wanapenda ushindani kwenye ligi.

Wachezaji wa Tabora United kwa walichokiona kiwe kama deni kwao, waendelee kucheza kwa nguvu na ari ile ile walioionesha kwenye mchezo dhidi ya Yanga, si baada ya hapo wanarudi tena kuwa kibonde kwani kufanya hivyo watakuwa hawajawatendea haki mashabiki wao.

Tunaamini hili pia litakuwa ni somo kwa timu zingine za Ligi Kuu hasa kwa kuangalia heshima, zawadi na mapokezi ambayo mashabiki wa soka waliokuwa wakiwaonesha wachezaji wa Tabora United kila wanapopita.

Hivyo hata zingine zinaweza kupata heshima hiyo kama viongozi na wachezaji wake watajitambua na kuweka mkazo kwenye kusaka ushindi dhidi ya timu zote zinazokutana nazo kwenye Ligi Kuu, zikiwamo zile kongwe na kubwa, Simba, Yanga na Azam FC.

Tunahitaji sana upinzani huu ili kuzidi kupandisha hadhi ya soka la Tanzania kwani pamoja na kutajwa kuwa linashika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu, lakini bado limekuwa la farasi wawili ambao ni Simba au Yanga ambao si tu kwamba zimekuwa zikipokezana ubingwa tangu msimu wa 2013/14, pia timu zingine ukiondoa Azam FC, zimekuwa hazioneshi hata dalili ya kusaka ubingwa.


Safari hii tumeona Singida Black Stars ikionesha imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kusaka ubingwa, ikiungana na Azam FC, hivyo kuwa na angalau timu nne zenye uzani wa juu.

Tunatarajia ushindani huu utazidi kuongezeka kadri ligi itakavyozidi kusonga mbele kiasi cha kuvutia zaidi, kusisimua kiasi kwamba msimu ujao wadhamini wengi wanaweza kujitokeza kwa wingi zaidi kuwekeza fedha zao na ligi kuendelea kupata umaarufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Makipa wazawa wanashawishi viongozi wa klabu kusajili wa nje

**NILIUTAZAMA** mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Fountain Gate iliyokuwa ikicheza nyumbani dhidi ya Pamba Jiji FC, nikakubaliana na mawazo ya viongozi wa klabu mbalimbali nchini kusajili makipa kutoka nje ya nchi.

Mechi hiyo iliyochezwa, Novemba 5, Uwanja wa Kwaraa, Babati mkoani Manyara, ilishuhudiwa, Fountain Gate FC ikipoteza kwa mara ya kwanza nyumbani kwao ilipochapwa mabao 3-1 dhidi ya Pamba Jiji, ambayo ilikuwa haijapata ushindi wowote kwa michezo 10 ya nyuma. Ukawa ni ushindi wa kwanza kwa timu hiyo.

Kilichovutia au kunishangaza ni jinsi mabao yalivyokuwa yakiingia. Yalikuwa ni mabao rahisi na ya kizembe kiasi kwamba unashangaa kama kweli anayefungwa ni golikipa wa hadhi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo ni ya sita kwa ubora Afrika.

Mfano mzuri ni bao la tatu, ambalo kwa hali ya kawaida halikutakiwa kufungwa hata kwa bahati mbaya.

Faulo ilitokea kwenye kibendera cha kona kuelekea kwenye lango la Pamba Jiji. Golikipa Bakari Fikirini, ndiye aliyekwenda kupiga. Cha kushangaza badala ya kuupiga mbele, aliupiga ndani, tena kule kule nyuma ya lango lake wakati yeye mwenyewe hayupo langoni.

Kilichotokea ni kwamba, mpira ule ulimkuta mchezaji wa Pamba Jiji akiwa na lango tupu akaukwamisha wavuni. Nadhani ni bao ambalo lilimkera kila shabiki wa Fountain Gate, pia kuwashangaza wengi uwanjani na waliokuwa wanautazama mchezo huo kupitia televisheni.

Hata kipa wa timu za mchangani hawezi kufanya hiki ambacho kipa huyu alikifanya katika mchezo huo.

Ingawa bado hazijathibitishwa, lakini habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema uongozi wa klabu hiyo umewasimamisha wachezaji wawili ambao ni golikipa Fikirini, Abal Kassim na kocha wa makipa, Ally Mustapha 'Barthez'.

Taarifa zinasema kusimamishwa kwao kunahusiana na mchezo huo, lakini mpaka sasa uongozi wa klabu hiyo haujatoa taarifa rasmi.

Ni kipa huyu huyu Fikirini, aliyewahi kudaiwa kufanya kosa lililoigharimu timu yake ya Ihefu FC ikafungwa na Yanga bao 1-0, Januari 16, 2023, katika mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Ligi Kuu msimu wa 2022/23.

Aliudunda mpira na kuuweka chini wakati nyuma yake kulikuwa na Fiston Mayele, akauwahi na kupachika bao pekee katika mchezo huo ambao kabla ya hapo ulikuwa mgumu na usiotabirika.

Kwa hili lililotokea naungana na baadhi ya viongozi wa klabu ambao wameanza kusajili makipa kutoka nje ya nchi.

Kuna mjadala ulizuka kwa baadhi ya wachambuzi wakihoji kwa nini kumekuwa na wimbi la kusajili magolikipa kutoka nje ya nchi, badala ya kusajili vipaji vilivyo hapa nchini.

Wakataka itungwe kanuni ambayo itafuta uwapo wa makipa wa kigeni nchi, badala yake wawe wazawa tu, ili wapate muda mwingi wa kucheza kwa ajili ya manufaa ya taifa.

Wasichokijua wachambuzi wengi ni kwamba viongozi wa klabu si kwamba wanakwenda kusajili makipa wa nje kwa sababu hapa nchini hakuna makipa bora au wazuri, bali ni wanatafuta uaminifu.

Baadhi ya makipa wazawa kwa sasa wamekuwa hawaaminiwi kutokana na tabia ya kile kinachoelezwa kuhujumu au kuuza mechi kwa timu pinzani, tofauti na makipa kutoka nje.

Wala si kwa bahati mbaya, Simba, Yanga, Azam na timu zingine kuwa na makipa kutoka nje. Wao wenyewe wanajuana na hawaaminiani.

Kwa hili lililotokea nadhani Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), na Bodi ya Ligi iendelee tu kuziruhusu klabu zinazotaka kusajili makipa kutoka nje ya nchi. Kingine ni kwamba hii ni kengele kwa makipa wazawa waanze kujitazama wenyewe na kujiuliza ni kwa nini kwa miaka ya hivi karibuni wameanza kutoaminika kukaa langoni hata kwa timu ndogo tu kama KMC, Coastal Union, au Namungo?

Hali ikiendelea hivi tusije kushangaa ukafika msimu klabu zote 16 zikawa na makipa wa kigeni. Wazawa sasa ni wakati wakujitafakari na kujirekebisha wenyewe, badala ya kusubiri kutungwa kanuni za kuwabeba.

# NMB yatenga milioni 450/- za kuhamasisha malipo kwa kadi

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB imezindua msimu wa sita wa kampeni maalumu ya kuhamasisha matumizi na malipo kwa njia ya kadi 'NMB MastaBata - La Kibabe,' ambayo kwa miezi mitatu mfululizo wateja wa benki hiyo watajishindia zawadi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 300, pamoja na safari za utalii wa ndani na nje ya nchi.

NMB MastaBata ni kampeni iliyoanza mwaka 2018, kabla ya kuboreshwa zaidi mwaka 2019 ilipoitwa MastaBata 'Sio Kawaida,' ikafuata MastaBata 'KivyakoVyako' mwaka 2020, kabla ya mwaka 2021 kuitwa Mastabata 'Kotekote,' na mwaka jana kutambuliwa kama Mastabata 'Halipoi.'

Uzinduzi huo uliosimamiwa na Ofisa wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Rasul Masoud, ulifanyika Mlimani City, Dar es Salaam juzi na kampeni hiyo itadumu hadi Februari 12 mwakani, siku ambayo washindi sita wa fainali na wenza wao watapatikana kwa safari ya Dubai kwa siku tano iliyogharamiwa na NMB.

Katika kipindi hicho, droo mbalimbali zitachezeshwa, ambako washindi 100 wa kila wiki watapokea Sh. 100,000 katika akaunti zao, huku washindi 30 wakijinyakulia Sh. 500,000 kila mwisho wa mwezi kwa miezi miwili na wengine 10 wakijishindia safari ya kwenda kutembelea Mbuga za Wanyama za Mikumi na Ngorongoro.

Kwa miaka sita, NMB imejikita katika kuhamasisha wateja wao wenye kadi za benki hiyo, kufanya malipo ya bidhaa, hotelini, migahawani, 'supermarket,' maeneo ya starehe na popote pale, huku ikitenga kitita cha fedha taslimu kama zawadi, bidhaa za zawadi na safari za kitalii ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Idara ya Kadi ya Benki ya NMB, Philbert Casmir, alisema kampeni hiyo itayofikia ukomo Februari 12 mwakani, ni kwa ajili ya wateja wenye kadi za NMB Mastercard, ama kadi ya aina yoyote inayotolewa na benki hiyo, huku akiwataka wasio na akaunti na kadi za NMB, kufungua sasa kampeni inapoendelea.

> **"Washindi zaidi ya 2,000 watapata nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 450, ambapo ili kushiriki kampeni hii utatakiwa kufanya ununuzi kwa kutumia kadi yako ya NMB Mastacard kwenye mashine za POS, kwenye mitandao (online) na Lipa kwa QR link.**

"Washindi zaidi ya 2,000 watapata nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 450, ambapo ili kushiriki kampeni hii utatakiwa kufanya ununuzi kwa kutumia kadi yako ya NMB Mastacard kwenye mashine za POS, kwenye mitandao (online) na Lipa kwa QR link.

"Katika kuhitimisha kampeni hii, washindi sita watajishindia tiketi za kwenda Dubai pamoja na wenza wao kwa siku tano, safari itakayogharamiwa kila kitu na NMB," alisema Casmir huku akibainsiha ununuzi huo utakaofanyika kwenye migahawa, 'supermarket,' vituo vya mafuta, maduka makubwa na sehemu za starehe.

"Faida za matumizi kwa njia ya kadi nyingi na tunatamani kuona kila mteja wetu ananufaika nayo, ambazo ni pamoja na urahisi wa kutumia bila kuwa na fedha taslimu mkononi, ambazo ni hatari kutembea nazo. Lakini hii inakupa fursa ya kuweka rekodi za matumizi ya fedha zilizomo katika akaunti," alibainisha Casmir.

Akizungumza katrika uzinduzi huo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, aliwataka watanzania kujitokeza kwa wingi kufungua akaunti ili kunufaika na huduma za NMB, zikiwamo promosheni mbalimbali zinazoendelea.

"NMB tunazo kampeni zinazowapa zawadi wateja wapya wanaofungua, kuna kampeni inayotoa zawadi kwa wateja wenye akiba isiyopungua Sh. 100,000, na leo tunakuletea kampeni hii ambayo inakuwazawadia unapotumia fedha zako kwa njia ya kadi tu, pale utapofanya ununuzi kwenye mashine za PoS au NMB Pay by Link. "Hii maana yake utafanya ununuzi wa bidhaa zako, na kukupeleka kwa safari za utalii wa ndani na nje ya nchi, na unaweza kujikuta ukishinda zawadi ya ada ya shule ya mtoto wako inayofikia Sh. milioni nne, ambazo zitakwenda kwa washindi wetu 10," alibainisha Mponzi.

Mponzi alibainisha kuwa katika droo za kila mwezi, washindi 10 watakaopatikana, watagawanywa makundi ya washindi watano watakaokwenda Mikumi na Ngorongoro kwa gharama za NMB, kama itakavyokuwa kwa washindi sita wa fainali na wenza wao, watakaopelekwa Dubai kwa siku tano.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

## Advertisements of Employment

1. **Transport Officer**

**Key Responsibilities:**

- Oversee daily operations of the transportation department, ensuring efficient fleet management.
- Plan and schedule transport routes, ensuring timely deliveries and optimal fuel usage.
- Manage vehicle maintenance and safety compliance, ensuring adherence to regulatory standards.
- Supervise and train transport staff (drivers, coordinators) to ensure high operational standards.
- Ensure all transportation records and logs are maintained accurately for audits and compliance.
- Address customer concerns regarding transportation services and resolve issues promptly.
- Track vehicle movements using GPS tracking devices and ensure no safety or route violation/deviation.
- Coordinate with GPS and other relevant fleet service providers to resolve all issues and maintain the highest customer standards.
- Prepare yearly, monthly, weekly and daily logistic plans to meet customer requirements.
- Prepare and report performance of the fleet daily, weekly, monthly and yearly and suggest improvements following the PDCA approach.

**Qualifications:**

- Bachelor's degree in Logistics, Transportation Management, or related field.
- At least 3 years of experience in a similar role, preferably in fleet management or transport operations.
- Strong understanding of transport regulations and safety standards.
- Excellent organizational and communication skills.
- Ability to solve complex problems and think critically under pressure.

√ Location: **Moshi.**

**Mode of Application:**

All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned, to reach him not later than 13/11/2024.

**The Managing Director, Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**hr@bbl.co.tz**
**MOSHI.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Mguli Petrol Station - Kibaigwa Majengo |
| **Nambari ya Leseni:** | PRL-2020-355 |
| **Mahali Kituo kilipo:** | Kiwanja Na. 2, Kitalu "Q" Eneo la Majengo Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma |
| **Jina linalopendekezwa:** | Kobil Tanzania Limited |
| **Mmiliki wa awali:** | Mguli Petrol Station |
| **Mmiliki mpya:** | Kobil Tanzania Limited |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe kuchapishwa kwa tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**
**Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli,**
**S. L. P. 2857, DODOMA**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**
**Namba ya Huduma kwa Wateja**
**0800110030**

**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA RIFT VALLEY (RIVACU LTD), S.L.P 50 BABATI**

**REG. 5459**

r.i.v.a.c.u info@rivacu.co.tz +255788449764

## MWALIKO WA ZABUNI

**Zabuni namba. 67/RIVACU/DSZ/2024/2025/G/01**

**KWAAJILI YA KUUZA GARI ISUZU HTR.**

**Tarehe 06/11/2024**

1. **RIFT VALLEY COOPERATIVE UNION (RIVACU LTD)** ni Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Manyara na sehemu ya Mkoa wa Arusha katika Wilaya ya Karatu. Chama kilisajiliwa Machi 31, 1988. Kwa sasa RIVACU LTD inafanya kazi katika Halmashauri za Babati(W), Babati(M), Mbulu(W), Mbulu(M), Hanang(W) na Karatu(W)

2. **RIVACU LTD** imepata kibali na ridhaa ya wanachama kwa kupitia Mkutano Mkuu wa 33 kuuza gari la chama kwa mujibu wa masharti ya chama, sheria na kanuni ya vyama vya Ushirika.

3. Mwenyekiti wa Bodi ya RIVACU LTD kwa niaba ya bodi anatangaza zabuni shindani ya Kitaifa (National Competitive Tender) kuuza gari linalomilikiwa na chama ISUZU HTR lenye CHASIS No. JALHTR11JJ3001115 na Usajili No. T 841 AHX lililopo katika Ofisi za RIVACU LTD Halmashauri ya Mji wa Babati.

4. **RIVACU LTD** inapenda kuwataarifu wananchi wote wenye uwezo wa kushiriki zabuni hii wanakaribishwa ili kushindana kwa uwazi kwa kuzingatia vigezo na masharti ya kuuza gari kwa njia ya zabuni hii kama ifuatavyo;

| NA | AINA YA GARI | NAMBA YA GARI | CHASIS NAMBA | INJECTION |
|---|---|---|---|---|
| | ISUZU HTR | T.841 AHX | JALHTR11JJ3001115 | DIRECT INJECTION |

5. **RIVACU LTD** inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wanunuzi kwa kutuma barua zenye bei zao mapema wakianisha na taarifa muhimu za waombaji zifuatazo; Anuani, namba za simu na barua pepe pamoja na vivuli vya nyaraka halali za usajili wa kisheria (kama mwombaji siyo mtu binafsi yaani taasisi, mashirika, kampuni, vyama, asasi n.k)

6. Mwombaji anayehitaji kuona au kukagua gari husika awasiliane na RIVACU LTD kupitia simu +255788449764 au +255784698505 barua pepe: rivacuunion@gmail.com. Muda wa kukagua utakuwa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 09:30 jioni kila siku kabla ya siku ya ufunguzi wa zabuni.

7. Nyaraka za zabuni pamoja na fomu za maombi ya zabuni pamoja na vielelezo vingine muhimu vinapatikana katika ofisi za RIVACU LTD zilizopo Mtaa wa Ngarenaro, Kiwanja Na.147 Kitalu "N" Babati mji karibu na kituo cha mafuta cha DASH PETROLEUM. Aidha waombaji watapaswa kulipa ada ya maombi kiasi cha shilingi 100,000/= (Laki moja) tu na kiasi hiki hakitarudishwa.

8. Mwombaji atakayeshinda zabuni atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi cha ofa aliyotoa ndani ya muda wa siku saba (7) baada ya kupewa taarifa rasmi kuwa ameshinda zabuni. Malipo yaliyosalia yaani asilimia sabini na tano (75%) yakamilike katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya kutaarifiwa kushinda zabuni na baada ya malipo kufanyika kwa 100% mnunuzi atapata kibali cha kuchukua na kumiliki mali hii. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa gari hilo na fedha alizolipa hazitarejeshwa ikiwepo ada ya maombi kiasi cha shilingi 100,000/= (Laki moja) pamoja na malipo ya awali yaani asilimia ishirini na tano (25%).

9. Zabuni zielekezwe kwa Meneja Mkuu, Makao Makuu ya RIVACU LTD, S.L.P 50, Babati-Manyara Mtaa wa Ngarenaro Block "N" Plot No.147 kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 09:30 jioni kuanzia siku ya Jumatatu hadi Ijumaa zikijumlishwa isipokuwa siku za Jumamosi, Jumapili na Sikukuu.

10. Muda wa mwisho kuwasilisha zabuni ofisini si zaidi ya tarehe 20/11/2024, Siku ya Jumatano kabla ya saa 4:00 asubuhi. Zabuni zitafunguliwa hadharani tarehe 20/11/2024 saa 4:30 asubuhi makao makuu ya RIVACU LTD, Mtaa wa Ngarenaro, Kiwanja Na 147, Kitalu "N"

11. Zabuni zilizochelewa au kutumwa kwa njia ya kielectroniki hazitapokelewa kwa tathimini bila kujali mazingira yeyote. Aidha zabuni hizo hazitafunguliwa wala kusomwa hadharani katika hafla ya ufunguzi wa zabuni.

Imetolewa na;

**YUDA P. SULLEY**
**MWENYEKITI WA BODI**
**RIVACU LTD.**


# RC kutoa chopa kudhibiti uharibifu wa mazingira



**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (pichani), ameahidi kutoa chopa kwa kikosi kazi cha kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo ya mito na mabonde jijini Dar es Salaam ili kutembelea Bonde la Mto Mpiji, Bonde la Mto Nyakasangwe, Bonde la Mto Tegeta na Bonde la Mto Msimbazi ili kuona na kuchukua hatua dhidi ya uharibifu unaofanywa katika mito hiyo.

Alitangaza hatua hiyo mwishoni mwa wiki wakazi akizindua programu ya upandaji miche ya michikichi 5,000 katika Mto Mpiji eneo la kata ya Mabwepande kwa kushirikiana na Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu, Kidakio cha Pwani, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Halmashauri za Manispaa za Ubungo na Kinondoni, makandarasi na vikundi cha Machepe ambao wanafanya kazi ya kusafisha mto kwa mujibu wa sheria.

Chalamila alisema Mto Mpiji ni miongoni mwa mito mikubwa kwa mkoa wa Dar es Salaam, lakini sasa kuna uharibifu mkubwa unaofanyika kutokana na kukithiri shughuli za kibinadamu na watu wanaodai ni wasafisha mito wasiofuata taratibu na sheria.

"Kile kikosi kazi kinachoshirikiana na NEMC na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, mkiwa tayari semeni, niwape helikopta ili na ninyi mpande kwa juu mwangalie mto huu (Mto Mpiji) ili mpate majibu mazuri juu ya uharibifu unaofanywa kwenye mto huu.

"Ninataka mtembee Bonde la Mto Mpiji, mtembee Bonde la Mto Nyakasangwe, mtembee Bonde la Mto Tegeta na mtembee Bonde la Mto Msimbazi mwone namna uharibifu ulivyofanyika," alisema.

Chalamila alisema kuwa kutokana na athari hizo, ofisi yake imeshirikiana na Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu, Kidakio cha Pwani, NEMC, ofisi ya mkuu wa wilaya na vikundi mbalimbali kutoa miche ya michikichi 5,000 kwa ajili ya kupandwa katika kingo za mto huo kuthibiti athari zitakazotokea.

Chalamila alisisitiza suala la utunzaji mazingira, hususani chanzo hicho cha maji na kuiagiza Wami/Ruvu kuweka uangalizi wa karibu na ufuatiliaji miche hiyo iweze kuleta tija na kutimiza malengo yaliyowekwa kwa serikali.

"Miti mingi ina faida, lakini tukasema miche ya michikichi ina faida nyingi. Watu wa bonde kwa kushirikiana na vijana wanaosafisha mito, tukasema kuna kipindi shughuli za usafishaji mito zinasimama kutokana na maji kuwa mengi, hii michikichi itakuwa inazalisha mafuta ya mawese na vikundi vitakavyonufaika ni hivihivi ambavyo vinasafisha mto huu," alisema.

Aliongeza kuwa wananchi wanapaswa kuchukua jukumu la kulinda miti hiyo mara baada ya kupandwa ili kuhakikisha ufanisi wake unadumu.

"Tunahitaji usimamizi na ufuatiliaji wa karibu kutoka kwa viongozi wa maeneo haya, kwa kushirikiana na jamii, ili kuifanya miti hii kuwa sehemu muhimu ya maendeleo yetu ya kiuchumi na kimazingira," alisema.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Elibariki Mmassy alisema kaulimbiu ya programu hiyo ni "Michikichi kwa Uhifadhi wa Mazingira na Uchumi Endelevu," kwa kuhakikisha mradi huo unaleta mabadiliko ya muda mrefu kwa mazingira na jamii ya eneo hilo.

Alisema miche hiyo ina umuhimu mkubwa katika kuhifadhi mazingira na maji, kwani inasaidia kudhibiti mmomonyoko wa ardhi na kuzalisha mafuta na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na eneo kwa ujumla.

Uzinduzi huo pia unakuja wakati ambapo maeneo mengi nchini yanakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, ukiwamo ukame na mmomonyoko wa ardhi.

Wataalamu wa mazingira wanasisitiza kuwa kupanda miti kunasaidia kuhifadhi unyevunyevu wa ardhi na kuongeza viwango vya mvua, jambo linalochangia kuboresha hali ya hewa.

Alisisitiza kuwa Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa eneo hilo kuhusu faida za michikichi na umuhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji kwa ujumla.







# Aliyeongoza kijiji kwa miaka 30 akatwa jina

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Kijiji cha Engonongoi Kata ya Terrat, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, kwa miaka 30 tangu mwaka 1995 hadi mwaka 2024, Nemamiyai Shinini, amelalamikia kamati ya siasa ya CCM Wilaya hiyo kukata jina lake.

Nemamiyai ambaye ni Laiboni, akizungumza na Nipashe jana, alisema alishinda kwa kupata kura 700 za maoni ya CCM ya kijiji hicho ila jina lake likakatwa.

Alisema baada ya kushinda jina lake liliwekewa alama nzuri kupitia vikao vya tawi na kata na kisha kupitishwa na kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya na kupewa barua ya uteuzi.

"Wakati najiandaa kwenda ofisi ya Kata ya Terrat kupeleka barua, ili kupata fomu za kuomba kugombea serikalini nikashangazwa kukatwa jina na mgombea wa pili kuteuliwa kugombea," alisema.

Alisema ameongoza kijiji hicho tangu kilipoanzishwa mwaka 1995, kutoka Kijiji cha Loswaki na kufanikisha maendeleo mengi ila hivi sasa ndiyo wanakata jina lake.

"CCM wilaya, waliniita na kudai kuwa sijui kusoma wala kuandika ila nikaandika jina langu na kuwasomea mbele yao, ila nikashangazwa na kukatwa jina langu," alisema Nemamiyai.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, amethibitisha kukatwa jina kwa mgombea huyo kutokana na kutojua kwake kusoma wala kuandika Kiswahili.

Laizer alisema baada ya kubaini kuwa mgombea huyo hajuwi kusoma wala kuandika, ikabidi wakate jina lake na kumteua aliyekuwa anafuata kwa kupata kura nyingi, kwani muda wa uchaguzi umepita.

"Ni utaratibu wa chama tu umetumika kwani kanuni na taratibu zinaeleza kuwa mgombea asiyejua kusoma na kuandika hawezi kupatiwa nafasi ya kuiwakilisha CCM," alisema Kiria.

Alisema hivi sasa wanajipanga baada ya kuanza kampeni wanatarajia kufanya mkutano na kuzungumza na wanachama wa Engonongoi ili kuwaelezea hali ilivyo.

Kadhalika, Alaice Mollel, alisema ni vyema Nemamiyai apumzike, kwani miaka 30 aliyoongoza inatosha anapaswa kuacha kijiti kwa mwingine.

"Kama hajui kusoma wala kuandika ni vyema akapisha wasomi wakaongoza kijiji, kwani miaka 30 aliyoongoza inamtosha hii mitano haitamsaidia chochote kipya atakachofanya," alisema.

Mkazi wa Wilaya hiyo, Lekaita Lekaita, alisema Nemamiyai ameongoza kijiji hicho kwa nidhamu, maadili, kutokula rushwa wala kuuza ardhi ya kijiji, ndiyo sababu anapendwa na kuchaguliwa.

"Kuna baadhi ya viongozi wa vijiji vingine hawajuwi kusoma wala kuandika na wameuza ardhi ya vijiji na bado tena wakapitishwa na CCM kugombea upya," alisema Lekaita. Mkazi mwingine wa Simanjiro, Mosses Ole Sanjiro, alimpa pole kwa kukatwa jina, ila anapaswa kuwapisha wengine kwani kuongoza kwa miaka 30 ni muda mrefu inatosha.

"Mzee wangu pole sana ila ukiendelea utakuwa kama Museveni japo una haki ya kuongoza kama watu wanakupenda ila CCM wamekufanya mbuzi wa kafara kwani wapo viongozi wa vijiji na vitongoji hawajui kusoma wala kuandika ila wameachwa wagombee," alisema.

Mkazi mwingine, Zephania Meshaki, alisema Nemamiyai ameonewa kwani wapo baadhi ya wagombea wakiwamo nafasi ya ujumbe wa serikali ya kijiji hawajui hata kiswahili ila wamepitishwa.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ilitembelea chanzo cha maji cha Jordom wilayani Hanang' mkoani Manyara, wakati ikikagua miundombinu ya maji iliyoharibiwa na maporomoko ya mawe na tope yaliyotokea Desemba 3, mwaka jana na namna ambavyo serikali imerejesha huduma. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Watafiti watakiwa kutoa matokea ya utafiti mapema kwa wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewakumbusha watafiti nchini umuhimu wa kutoa matokeo ya utafiti wao kwa jamii, ili kuwezesha wananchi kunufaika nayo katika kuhakikikisha uchumi unakua na utatuzi wa changamoto za kijamii na taifa.

Aidha, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizopiga hatua kubwa katika kujenga uchumi hasa katika sekta ya miundombinu, afya, umeme na nyinginezo hivyo ni vema tafiti zitoe taarifa za ukuaji uchumi, ili kuonyesha nchi inavyopiga hatua ya kimaendeleo katika nyanja mbalimbali.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

Alikuwa akifungua kongamano la tatu la kimataifa la usimamizi wa biashara na ukuaji wa uchumi lilioandaliwa na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).

Simbachawene, alimwakilisha Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko.

Alisema katika ushindani wa uchumi utafiti ndio unaweza kuleta maendeleo kwa kutumia tafiti zinazofanywa na watafiti wa ndani, katika sekta mbalimbali na kutoa matokeo chanya yanayotokana na tafiti atamizi zinazotatua changomoto za wananchi na si kubaki katika makabrasha pekee.

"Kumekuwa na tabia ya watafiti kuzifungia katika kablasha tafiti zetu hakuna anayezijua, lakini pia wengi tumejenga tabia ya kuzidharau tafiti za wazawa wakati nyingi zinatoa majibu ya changamoto tulizonazo naomba tuzitoe, ili tupige hatua kubwa za kiuchumi na kusaidia utatuzi wa matatizo katika jamii," alisema.

Alisisitiza kuwekeza zaidi katika tafiti zenye tija, ili kutoa matokeo ya changamoto zilizopo kwa kutoa matokeo ya tafiti zinazofanywa kwa wananchi na kuwaomba Watanzania kuamka na kuamua kuzitumia tafiti za wazawa, ili kupata ufumbuzi wa changamoto zilizoko.

"Tanzania tumepiga hatua kubwa za kimaendeleo lakini watafiti hawaziweki tafiti zilizofanyika hadi kupiga hatua na kuzielezea, hivyo ni vema watafiti kwenda kiuhalisia zaidi na kutoa majibu ya tafiti zilizofanywa, ili kusaidia jamii kutatua changamoto zilizoko katika sekta mbalimbali na serikali tuzifanyie kazi ili kukuza uchumi," alisema.

Aidha, alishauri watafiti wanaogundua vitu mbalimbali kuendelezwa kwa kutafutiwa soko, badala ya wahusika wa ukusanyaji mapato kuwakandamiza na kufifisha bunifu zao, kwa sababu kugundua na kuvumbua si habari ya sera bali wanapaswa kuendelezwa zaidi.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, alisema ni wakati muafaka wa tafiti zinazotolewa na wataalamu hao kuanzia kuzitumia kwa wananchi, ili kuleta tija katika maendeleo sanjari na kudadavua kwa kina juu ya mwelekeo wa uchumi haswa katika ubunifu wa biashara na uchumi, hususan katika tafiti atamizi.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea katika kuboresha mifumo ya kisera hasa za mapato na matumizi, nishati na miundombinu katika kuongeza kasi ya shughuli za kibinadamu na upunguzaji wa kiwango cha umaskini.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uhasuri ya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Prof. Jehovaness Aikael, alisema mtaji na ubora wa rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika kuhakikikisha ukuaji wa uchumi, ikiwemo mchakato wa kuongeza pato halisi la Taifa na la mtu mmoja mmoja, ikiwemo ongezeko la uwezo wa uchumi katika kuzalisha bidhaa na mabadiliko ya ubora wa watu.

# TASAF yatoa Sh. milioni 981 Arusha

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

SERIKALI imeendelea kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia mradi unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kwa kutoa fedha Sh. milioni 981.3 kwa walengwa walioko kwenye mpango huo katika Mkoa wa Arusha.

Akizungumzia juzi na Nipashe, Mratibu wa TASAF, Mkoa wa Arusha, Richard Nkini, alisema kiasi hicho cha fedha kimetolewa kwa kaya 41,272, ikiwa ni ruzuku ya mwezi Julai na Agosti 2024 kwa halmashauri zote saba zilizoko mkoani humo.

Mratibu huyo alisema fedha hizo ni mahsusi kwa ajili ya ruzuku ya msingi, elimu pamoja na afya ili kuhakikisha walengwa hao, wanapata mahitaji yao ya msingi, ikiwa ni pamoja na watoto wa kaya hizo, kupata mahitaji muhimu ya kuwawezesha kuhudhuria masomo na kliniki kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

"Fedha hizi licha ya kuwasaidia walengwa kupata mahitaji ya familia, lakini zaidi zinawawezesha kuanzisha miradi midogo midogo ya kuinua pato la familia na hatimaye kutoka kwenye wimbi la umaskini uliokithiri," alisema Nkini.

Hata hivyo, wanufaika hao wameishukuru serikali kwa kuendelea kuwajali wananchi wa kipato cha chini, kwa kuwa kabla ya kuwepo kwa mradi huo wengi walishindwa kuendesha maisha yao na familia zao, kutokana na hali ngumu maisha iliyosababishwa na kipato duni.

Mmoja wa wanufaika hao, Zuhura Ally, Mkazi wa Kata ya Ngarenaro, alisema kupitia fedha hizo amefanikiwa kuwasomesha wajukuu wake, ambao ni yatima kwa kuwanunulia mahitaji ya shule na kuwapatia matumizi, huku akitumia fedha nyingine kwa ajili ya matumizi ya familia, jambo ambalo hapo awali ilikuwa ni ngumu kwake na familia.

"Ninaishukuru serikali kwa kutujali, mimi ninalea wajukuu wangu ambao ni yatima, ninamshukuru Mungu, huu mradi wa TASAF umetusaidia wengi, kabla ya hapo tulikuwa na hali ngumu ya maisha," alisema Zuhura.





# Wahitimu TASAF wagoma kuondolewa kwenye ruzuku

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAHITIMU 34 kati ya 4,000 waliokuwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), mkoani Shinyanga, wamegoma kuondolewa kwenye mpango huo kwa madai bado ni masikini na hawana uwezo wa kula milo mitatu kwa siku.

Wahitimu hao akiwamo Amina Juma kutoka mtaa wa Majengo, Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga waliiambia Nipashe juzi kuwa licha ya kutokumudu milo miwili vilevile hawana uwezo wa kutafuta mahitaji ya familia zao hasa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Amina alisema alipewa taarifa ya kuondolewa kwenye mpango huo akiwa bado masikini hivyo kuiomba serikali kuendelea kumuhudumia mpaka pale atakapokuwa na uwezo lengwa katika mpango huo.

Naye Sambi Mandalu kutoka Mtaa na Kata ya Kolandoto alisema, ni kweli alifanyiwa tathimini na alijibu maswali vema aliyokuwa anaulizwa na maofisa wa TASAF, lakini amekuja kuambiwa kuwa ni mhitimu na hana sifa ya kupokea ruzuku.

Ofisa ufuatiliaji wa TASAF katika Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Shinyanga, Tabu Maro, alikiri kuwapo kwa baadhi ya wahitimu wa TASAF waliogoma kuondolewa kwenye mpango kwa kigezo cha bado ni masikini, huku kwenye tathimini walijibu maswali yao vema na kuonekana hawana sifa ya kupokea tena ruzuku hiyo.

**Ofisa ufuatiliaji wa TASAF katika Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Shinyanga, Tabu Maro, alikiri kuwapo kwa baadhi ya wahitimu wa ....**

Alisema jumla ya kaya 4,000 zimehitimu na kuondolewa kwenye mpango kati yake 1,500 wanatoka Manispaa ya Shinyanga na 2,500 Wilaya ya Shinyanga, lakini 34 wamegoma kuondoka kwa kigezo kuwa bado ni masikini na kati yake 22 wanatoka Manispaa na 11 wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Maro alisema, sasa wanakimbilia ofisi za mkuu wa mkoa na wilaya kuomba wasiondolewe na malalamiko yao wameshayaripoti makao makuu ya TASAF kuangalia namna ya kuwarejesha au laah na hakuna anayeendelee kupokea ruzuku yoyote kwa kuwa malalamiko yao bado hayajatolewa uamuzi wowote tangu Agosti, 2024 yaliporipotiwa kwa mara ya kwanza.

Mhitimu Farida Hamisi (67) mkazi wa Ndala alisema, yeye alianza kupokea Sh.44,000 mwaka 2014 na kuzielekeza kwenye ufugaji wenye tija wa bata na alipopata bata 90 aliwauzia wazungu na kila moja kwa Sh.35,000 na kuanzisha ujenzi na nyingine kwenye biashara na sasa anauwezo wa kula milo mitatu, makazi mazuri ya kuishi na amekubali kuondolewa kwenye kupokea ruzuku.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani jijini Mwanza, Ally Charo, akitoa elimu ya usalama barabarani jijini humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lita za maziwa milioni 400 zazalishwa Mwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SERIKALI mkoani Mwanza imesema kwa kipindi cha mwaka 2023/24 uzalishaji wa maziwa mkoani humo umefikia lita milioni 398.53 na kuwa hatua hiyo imesababishwa na maboresho ya mazingira katika ufugaji wenye tija.

Kauli hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Katibu Tawala Mkoa Peter Kasere, wakati akifungua kikao kazi kati ya Bodi ya Maziwa na wadau wa maziwa mkoani hapa kilicholenga kutoa maelekezo juu ya uzingatiaji wa sheria za usajili wa biashara na taratibu za kuomba vibali ili kukuza na kufanya biashara yenye tija.

Kasere alisema licha ya kiwango hicho kikubwa cha uzalishaji maziwa ni wastani wa asilimia 0.6 pekee yanayosindikwa kupitia viwanda vidogo vidogo vilivyopo mkoani hapa.

Alisema katika jitihada za kuimarisha tasnia ya Maziwa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza umejielekeza katika kuboresha mazingira ya ufugaji wenye tija na kuhakikisha uwekezaji wa viwanda vya kusindika maziwa unakuwa mkubwa.

"Mpaka sasa mkoa una jumla ya mashamba makubwa 15 ya ng'ombe wa maziwa na chama kikubwa cha ushirikika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa cha UWAWAMWA, ambacho kimeanza kuchakata mtindi na yogati na kuna jumla ya viwanda vidogo 13 vya kuchakata maziwa vimeanzishwa," alisema.

Aidha, alisema jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha kilimo cha malisho bora ya ng'ombe, upatikanaji wa pembejeo za kilimo sambamba na kuendeleza jitihada za uanzishwaji wa Kiwanda cha Maziwa cha Mabuki.

Ofisa Sheria Bodi ya Maziwa Tanzania, Haruna Maarufu, alisema wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia sheria, ikiwa ni pamoja na kufanya usajili wa biashara zao kuepukana na adhabu mbalimbali wanazoweza kutozwa kwa mujibu wa sheria ya maziwa sura 262 ya mwaka 2004 kifungo 17(1) na 17(2) na kanuni ya usajili wa wadau wa wadau maziwa ya mwaka 2007 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2020 kifungu cha 4(1) na 4(2).

Ofisa Masoko kutoka bodi hiyo, Hamisi Kiimbi alisema serikali inatoa vibali vya kutoa au kuingiza maziwa nchini kwa wafanyabiashara, ili kulinda afya za walaji pamoja na kuweka ukomo wa bidhaa hiyo sokoni.

Mfugaji wa ng'ombe Rehema Mwalugala aliomba serikali pamoja na bodi hiyo kuweka mkakati mahusus wa kutoa elimu kwa wafugaji, ili kuboresha ufugaji na kupata maziwa bora.

# Diwani aomba boti ya wagonjwa

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

DIWANI wa Bugoro, visiwa vya Kome na Masome, Halmashauri ya Buchosa mkoani Mwanza, Mussa Ngazira ameomba serikali kupeleka boti ya wagonjwa yenye mwendo kasi, ili kuwanusuru wananchi wa visiwani humo kwa kuwawahisha wagonjwa wanaopewa rufani katika Hospitali ya Rufani Wilaya.

Ngazira alitoa ombi hilo juzi katika Baraza la Madiwani kwenye kipindi cha maswali ya papo kwa papo na kuhoji ni lini serikali itapeleka 'speedboti' visiwani humo, ili kunusuru maisha ya wananchi wakiwamo mama wajawazito na watoto wanaopewa rufani kwenda Hospitali ya Isaka au Sengerema.

Alisema kituo hicho chenye wakazi 57,761 kina kituo kimoja cha afya hali ambayo inasababisha kuzidiwa na wagonjwa huku wanaopewa rufani wakiwa hatarini kupoteza maisha kutokana na kukosa usafiri wa uhakika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Buchosa, Benson Mihayo, alisema halmashauri imepeleka maombi kwa ajiri kupata gari za wagonjwa mbili ambapo moja itatumika katika kisiwa cha Kome na nyingine Maisome na tayari mchakato huo upo hatua nzuri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Buchosa, Idama Kibanzi alisema Mkurugenzi anatakiwa kutazama kwa upya sehemu zote ambazo zinahitaji vivuko kwa kusaidia wagonjwa kwani Maisome na Kome vinatakiwa kuwa na huduma ya kutosha na vituo kufanya kazi ili kupunguza adha ya wajawazito kupoteza maisha kwa ajili ya kwenda vituo vya afya ambavyo lazima uvuke maji

Aidha, Idama alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanadhibiti vifo vya wamama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kukosa boti ama kupoteza maisha kwa kokosa usafiri wa kuvuka kwa haraka ili kunusuri maisha yao.

Ikumbukwe ndani ya mwaka 2024 kinamama watatu wamepoteza maisha kwa kukosa usafiri licha ya kuwa wao ndio tegemezi katika jamii na familia zao.

Nipashe
Spotika




JUDE BELLINGHAM ALIWANYAMAZISHA WALIOKUWA NA SHAKA .. UK. 14




# SLOT ALIVYOTHIBITISHA UBORA WAKE LIVER

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp alipotangaza kuondoka kama kocha wa Liverpool mapema mwaka huu, wasiwasi ulijaa uwanjani Anfield.

Mjerumani huyo alikuwa gwiji wa Merseyside kutokana na ushindi wa Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kuondoka kwake kumekuwa sasa kunaonekana si pengo kutokana na uwapo wa Arne Slot.

Mholanzi huyo sasa ameshinda mechi 14 kati ya 16 za kwanza akiwa kocha wa Liverpool.

Slot alitoa dalili wazi kwamba wababe hao wa Ligi Kuu walipata uamuzi wao wa kocha msimu wa majira ya joto kwa kuwararua Leverkusen katika ushindi wa mabao 4-0.

Huku Diogo Jota akiwa nje na Darwin Nunez akiwa hana shauku, Luis Diaz alikabidhiwa funguo za nafasi ya mshambuliaji wa Liverpool, akifunga mabao matatu katika kipindi cha pili na kuiwezesha timu yake kupata ushindi.

Raia huyo wa Colombia kwa kawaida alijipenyeza kwenye maeneo mapana na akatafuta kauta, lakini uchezaji wake na ustadi wake uliwachanganya sehemu tatu za nyuma za Leverkusen, ambao mara chache walionekana kustarehe katika safu ya ulinzi.

Uamuzi wa busara ulionekana kuwashika wageni wa Alonso, bila suluhu ya kuzuia ghasia za Diaz kujitokeza.

Utambulisho wa Alonso hauna uwazi katika usiku mkubwa wa Ulaya, Ilikuwa daima kuchukua juhudi kubwa kwa Leverkusen kurudia ushujaa wao wa 2023/24 wakati huu.

Walipoteza mchezo mmoja pekee katika mashindano yote msimu uliopita - hiyo ikiwa fainali ya Ligi ya Europa - lakini kushindwa huku kunamaanisha kuwa tayari wamevuka idadi hiyo msimu huu.

Ni vigumu kwa Alonso kuwa na hofu, lakini hakuna shaka kikosi chake kinatatizika kukuza utambulisho wazi, huku Mhispania huyo akijaribu kuboresha safu yake ya ulinzi, lakini akifanya hivyo kwa gharama ya safu yake ya mbele ya ubunifu na hatari.

> **Mabingwa hao wa Bundesliga bado wako katika na fasi nzuri kwenye Ligi ya Mabingwa, lakini wako pointi saba nyuma ya Bayern Munich katika Ligi Kuu Ujerumani, huku kukiwa na nafasi chache za kutekeleza zinazoruhusu wa ikiwa Leverkusen itahifadhi taji lao la nyumbani.**

Majina ya makocha wote wawili yaliimbwa na umati wa Anfield.

Kwa kuzingatia nafasi yake kwenye timu mashuhuri ya Liverpool katika miaka ya 2000, haishangazi kwamba Alonso alipata upendo kutoka kwa umati wa nyumbani.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 42, alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2005 wakati wa mechi zake 210 Merseyside na kuvutiwa na umati wa Anfield kulionekana.

Walikuwa kimya sana kipindi cha kwanza huku Leverkusen wakiwakatisha tamaa wenyeji wao, ingawa ukimya huo uligeuka kuwa makofi ya nderemo kwa kila bao lililoingia.

Ni wazi Alonso bado anaheshimika katika klabu yake ya zamani na bado kunaweza kuwa na muungano katika siku zijazo.

Hata hivyo, kabla ya kukutana tena, sifa zinapaswa kutolewa kwa kocha wa sasa wa Liverpool.

Mabosi wachache wamefanya matokeo ya ajabu katika klabu kubwa, huku Slot mbunifu akianza na kuwaona 'Wekundu' hao wakiwa kileleni mwa jedwali za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Kushuka kwa kiwango fulani kulitarajiwa baada ya kuondoka kwa Klopp, lakini kama kuna lolote Mholanzi huyo ameipa nguvu timu yake mpya na kuwaunganisha katika harakati za kutafuta medali.

Slot mwenyewe alidai kuwa Liverpool hawakukabiliwa na upinzani wa hali ya juu wakati wa mwanzo wake mzuri, lakini wiki za hivi karibuni wamepata ushindi dhidi ya Chelsea, Brighton & Hove Albion na Leverkusen.

Hilo limechochea tu nia ya mapambano makubwa yajayo Real Madrid na Manchester City, michezo ambayo bila shaka itaashiria zaidi kuhusu sifa za Slot.

## ISIKUPITE

KIKOSI cha Pep Guardiola, Manchester City, sasa kimepoteza mechi nne mfululizo (mbali ya kupitia mikwaju ya penalti), hii ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika miaka 17 ya maisha yake ya ukocha, na hii ni mara ya kwanza kwa City kupoteza mechi nne kwa miaka 18, tangu Stuart Pearce alipokuwa anainoa. Katika wiki za hivi karibuni, wamepoteza kwa Bournemouth na Brighton kwenye ligi, Tottenham kwenye Kombe la Carabao, na Sporting kwenye Ligi ya Mabingwa.



## Extra Time



SON

# MABAO 8 YA HARAKA ZAIDI YA KAUNTA EPL

**LONDON,** England

KATIKA soka makocha wanatumia muda na nguvu zinazoongezeka kuweka timu zao ili kusambaratisha upinzani kupitia mbinu tata za pasi, na mashambulizi ya haraka ya kaunta.

**Pep Guardiola aliwahi kupongeza Bundesliga kama nyumba ya timu hatari zaidi duniani za mashambulizi ya kaun ta, lakini kundi la timu za Ligi Kuu England (EPL), zimezalisha msururu wa kasi ya kusumbua kufikia sasa msimu huu.**

Makala haya kwa msaada wa 90min inakuchambulia mabao nane ya haraka ya kaunta, twende sasa...

**8. Kaoru Mitoma (Brighton)**
**Muda: Sekunde 16.13**
**Mpinzani: Everton (Agosti 17)**

"Kutisha", ndilo neno Sean Dyche alichagua kuelezea kufungwa timu yake ya Everton ilikumbana nayo wikendi ya ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu England.

Brighton waliibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika Uwanja wa Goodison Park, na kupata ushindi kwa bao la kwanza la Kaoru Mitoma.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Japan alimaliza hatua hiyo sekunde 16 tu baada ya kushinda mpira ndani ya eneo la hatari la timu yake.

**7. Cole Palmer (Chelsea)**
**Muda: Sekunde 13.84**
**Mpinzani: West Ham (Septemba 17)**

Shauku ya mbio za kurejea kwa West Ham ilikuwa imeanza kufifia mapema dhidi ya Chelsea kwenye Uwanja wa London.

Palmer alifunga bao la mapema zaidi kwa vijana hao wa kocha, Julen Lopetegui waliokosa uchezaji tayari walikuwa chini kwa mabao 2-0 na akili imevurugika wakati Nicolas Jackson alipoanza harakati zake za kushambulia mwanzoni mwa kipindi cha pili.

Baada ya kukataa bila mpangilio nafasi ya kukamilisha hat-trick yake, Jackson aliweka mpira kwenye lango na kuweka msumari wa mwisho kwenye jeneza la West Ham.

**6. Jarrod Bowen (West Ham)**
**Muda: Sekunde 13.62**
**Mpinzani: Crystal Palace (Agosti 24)**

Mwisho mzuri wa kumaliza ushindi wa mabao 2-0 wa West Ham dhidi ya Crystal Palace haukuwa wakati wa kupendeza zaidi wa Jarrod Bowen alasiri pale Selhurst Park.

Wakati wachezaji wa West Ham wakishangilia bao la kwanza la Tomas Soucek, mkusanyiko wa matangazo ulikunjwa juu ya mvulana aliyeketi kando ya uwanja. Bowen alimtoa mtoto kwa haraka ili asipate madhara na kumpa shati lake la mechi mwishoni mwa mchezo.

**5. Mohamed Salah (Liverpool)**
**Muda: Sekunde 12.94**
**Mpinzani: Brighton (Novemba 2)**

Rekodi ya Arne Slot rekodi ya kupindua umiliki katika Liverpool imefafanuliwa kwa kudhibitiwa zaidi. 'Wekundu' hao wamepunguza kasi ya hali ya juu ya utawala wa Jurgen Klopp.

Mohamed Salah aliifungia Liverpool dhidi ya Brighton baada ya sekunde 13 akifunga kwa mguu wake wa kushoto na kuukunja mpira kwenye kona ya juu kwa mwendo ambao Slot aliuita "Mo Salah Special".

Kocha huyo Mholanzi kwa kufaa aliongeza: "Si mara ya kwanza na si mara ya mwisho kufunga kutoka nafasi hiyo."

**4. Nicolas Jackson (Chelsea)**
**Muda: Sekunde 12.15**
Mpinzani: Newcastle (Oktoba 27)

Cole Palmer hatahesabiwa kuwa ndiye aliyetoa pasi ya bao la kwanza la Nicolas Jackson dhidi ya Newcastle United, lakini anastahili takriban sifa zote kwa ajili ya kupanda uwanjani. Akichana kati ya safu nyeusi na nyeupe na bembea moja ya kiatu chake cha kushoto, Palmer nusura amlazimishe Pedro Neto kupiga pasi ya mraba kwa mshambuliaji anayeongoza wa Chelsea.

Palmer angefunga bao la ushindi, lakini ilikuwa pasi yake ya kuudhi ambayo Enzo Maresca aliitaja kama "sababu ya watu kulipa" kwenda Stamford Bridge. "Wanataka kumwona mchezaji wa aina hiyo."

**3. Son Heung-min (Tottenham**
**Muda: Sekunde 11.11**
**Mpinzani: West Ham (Oktoba 19)**

Son Heung-min alichambua kwa haraka hatua ya mshangao hadi kupata ushindi wa mabao 4-1, akifunga bao la tatu la mlipuko wa dakika nane na kuwazamisha West Ham.

Shambulizi kali la Tottenham la kukamilisha kipigo cha pili lilitazamwa na wachezaji watatu wa akiba wa West Ham ambao pia walikuwa wakisubiri kwa subira kwenye mstari wa kugusa huku Spurs wakifanya matokeo kuwa 3-1 dakika tano mapema.

**2. James Maddison (Tottenham)**
**Muda: Sekunde 10.6**
**Mpinzani: Brentford (Septemba 21)**

Brentford wamekuwa waanzilishi wa haraka zaidi wa ligi msimu huu. Bao la kwanza la Bryan Mbeumo dhidi ya Tottenham Hotspur katika mechi ya Septemba lilikuwa la pili kati ya mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu ambazo 'Nyuki' hao walifunga katika dakika ya kwanza.

Hata hivyo, Spurs walipata ahueni na kuongoza 2-1 hadi muda wa mapumziko na kubeba pointi zote tatu kwa shambulizi la haraka la James Maddison la dakika ya 85.

**1. Luis Diaz (Liverpool)**
**Muda: Sekunde 7.75**
**Mpinzani: Brentford (Agosti 25)**

Mechi ya kwanza ya Arne Slot nyumbani kama kocha wa Liverpool alitoa shambulizi la kushtua ambalo Jurgen Klopp angejivunia.

Mohamed Salah alikuwa wa kwanza kwenye mpira wa pili kutoka kona ya Brentford, akilazimisha mpira kupita kwenye njia ya Diogo Jota ambaye alionesha uvumilivu wa kutosha kabla ya kumtelezeshea Luis Diaz kwenye eneo la hatari.


Fowadi huyo wa Colombia alikuwa mnufaika wa mapema wa vikao vya kina vya mazoezi ya Slot na amemsifu kocha huyo wa Uholanzi kama "wa kuvutia".

## Nukuu

"Ukitaka kushinda kwenye mchezo wa soka, ni lazima uwe na uwezo wa kununua wachezaji ghali na kuwalipa mishahara mikubwa," **Rais wa Heshima, Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohamed 'Mo' Dewji.**



"Huu ni mchezo. Michezo si kila wakati jua linachomoza. Si wakati mzuri kila wakati. Leo kwenye mkutano na waandishi wa habari niliulizwa ikiwa ni mwisho wa enzi. Najua watu wanataka hivyo. Nasikia harufu ya hilo miaka mingi sana. Labda baada ya miaka saba kushinda Ligi Kuu mara sita, labda mwaka mmoja timu nyingine inastahili," **Kocha wa Machester City, Pep Guardiola, baada ya kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Brighton juzi.**



"Ikiwa tuko kileleni mwa ligi kwa alama tano, basi inamaanisha kitu, lakini tunapaswa kwenda hatua kwa hatua. Kama ungeniuliza kabla ya msimu kuanza nisingesema tulikuwa wagombea [ubingwa], lakini sasa inaonekana kama [sisi tupo kwenye mbio hizo]," **Kiungo mshambuliaji wa Liverpool, Alexis Mac Allister, baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Aston Villa juzi.**






Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua (kulia) raia wa Ivory Coast, akipambana na winga wa Tabora United raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne, kuwania mpira katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Alhamisi iliyopita, Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam. Mechi hiyo ilimalizika kwa Tabora United kushinda mabao 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

# VIPIGO VITANO VIKALI KWA YANGA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MOJA ya matukio ya kushangaza na kukumbukwa kwenye Ligi Kuu Tanzania wiki hii ni Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, kufungwa mara mbili mfululizo kitu ambacho kimewaacha mdomo wazi mashabiki na wapenzi wa timu hiyo.

Ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC Jumamosi ya Novemba 2, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, kabla ya kuchabangwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, Alhamisi iliyopita.

Kipigo cha pili ni kikubwa zaidi kwa timu hiyo, ambapo si mara nyingi sana kwa timu kubwa kama Simba na Yanga kupoteza kwa idadi kubwa kama hiyo ya mabao.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Offen Chikola, dakika ya 19 na 45 na la Nelson Munganga, dakika ya 78, huku Clement Mzize akifunga bao la kufutia machozi dakika za majeruhi, Tabora United ikiibuka na ushindi wa 3-1.

Kilikuwa ni kipigo kikubwa cha sita kwa timu hiyo kwa misimu 17 iliyopita ya Ligi Kuu.

Katika makala haya tunakuletea matokeo ya mechi ambazo Yanga ilikumbana na vipigo vikubwa zaidi, vitano kwenye Ligi Kuu kuanzia msimu wa 2008/09...

**1# Yanga 4-5 Villa Squad (2008/09)**

Ulikuwa mchezo wa mwisho wa kumaliza Ligi Kuu msimu wa 2008/09, uliochezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Yanga ilipokubali kipigo cha mabao 5-4 dhidi ya Villa Squad iliyokuwa ikijipapatua kubaki Ligi Kuu.

Mechi hiyo ilichezwa Aprili 27, 2009, ambapo mabao ya washindi yalifungwa na Chesido Mathew aliyepachika mawili, Jackson Makweta, Mau Aniu na Ally Msigwa.

Mabao ya Yanga yalifungwa na Boniface Ambani aliyefunga mawili, Bernad Mwalala na Idd Moshi.

**2# Yanga 3-4 Simba (2009/10)**

Msimu uliofuata, Yanga ilikutana na kichapo kingine kikubwa cha mabao 4-3 dhidi ya watani wao wa jadi, Simba, mechi ikichezwa, Aprili 18, 2010, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ulikuwa ni msimu wa Ligi Kuu 2009/10, huku mabao ya washindi yakifungwa na Uhuru Selemani, Mussa Hassan Mgosi aliyepachika mabao mawili, na Hillary Echessa aliyefunga bao la ushindi dakika za majeruhi.

Mabao ya Yanga yaliwekwa kwenye nyavu na Jerry Tegete, aliyefunga mawili, na Athumani Idd 'Chuji.'

**3# Yanga 0-5 Simba (2011/12)**

Kipigo kingine kikubwa ilichokipata Yanga, kilikuwa tena dhidi ya Simba, safari hii ulikuwa ni msimu wa 2011/12 wa Ligi Kuu, mechi ikichezwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Ilichezea kipigo cha mabao 5-0, mchezo ukipigwa, Mei 5, 2012, ambapo Simba ilipata mabao yake matatu kwa mikwaju ya penalti zilizofungwa na Felix Sunzu, Juma Kaseja na Patrick Mafisango na zote zilipatikana baada ya mchezaji hatari kipindi hicho aliyekuwa akicheza kama winga, wakati mwingine straika, Emmanuel Okwi, kuangushwa ndani ya eneo la hatari. Mganda huyo alifunga mabao mengine mawili katika mchezo huo.**

**4# Yanga 0-3 Mtibwa Sugar (2012/13)**

Wakati ikiongozwa na kocha Mbelgiji, Tom Saintfiet, Yanga ilikumbana na kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, msimu wa 2012/13, katika mchezo uliochezwa, Septemba 19, 2012, Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

Dakika ya 12 tu, Dickson Daudi aliifungia Mtibwa bao la kwanza, kabla ya straika tegemeo wa timu hiyo wakati huo ambaye baadaye alihamia Yanga, Hussein Javu, kufunga mabao mengine mawili, dakika ya 45 na 77.

**5# Yanga 0-3 Kagera Sugar (2019/20)**

Ilikuwa ni Januari 15, 2020, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Yanga iliangukia pua kwa kuchabangwa mabao 3-0 dhidi ya wageni Kagera Sugar.

Mbelgiji Luc Eymael ndiye aliyekuwa akiifundisha timu hiyo, ambayo ilishindwa kuwazuia vijana wa Kagera Sugar kupata ushindi mnono katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20.

Yusuph Mhilu, aliipatia Kagera Sugar bao la kwanza dakika ya 13, kabla ya Ally Ramadhani 'Kagawa' kufunga bao la pili na aliyeshindilia msumari kwenye jeneza la Yanga, alikuwa ni Peter Mwalyanzi, akifunga bao la tatu.

**JE, WAJUA?**




JUDE Bellingham aliwanyamazisha waliokuwa na shaka na kumaliza ukame wake wa mabao wa siku 179 baada ya kufunga bao zuri dhidi ya Osasuna wakati wa ushindi wa mabao 4-0 Jumamosi. Kabla ya ushindi wa Jumamosi, mara ya mwisho Bellingham kufunga ilikuwa wakati Real Madrid iliposhinda 5-0 dhidi ya Alaves Mei mwaka huu na msimu huu amecheza mechi 16 bila kuziona nyavu.





## ‘Wakulima tumieni mbegu za karanga zilizofanyiwa utafiti’

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) amewataka wakulima kutumia mbegu za karanga aina ya tarika moja na tarika mbili zilizofanyiwa utafiti na wataalamu wa kilimo, ili kuzalisha kwa wingi zao hilo nchini.

Dk. Thomas Bwana alitoa rai hiyo jijini hapa juzi wakati wa mkutano ulioandaliwa na Kituo cha Kimataifa cha Uboreshaji Mahindi na Ngano kwa kushirikiana na TARI Naliendele.

Alisema mbegu aina hiyo baada ya kufanyiwa utafiti na wataalamu wa kilimo kutoka TARI zimeonekana kuzalisha mazao mengi, kutokana na kuwa zinauwezo wa kuvumilia changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo ni vema wakatumia hizo, pindi msimu wa kilimo utakapowadia.

“Nawashauri wakulima watumie mbegu hizo za kilimo, tunahitaji kuona wakulima wa zao hilo wanapiga hatua kwenye kilimo wanachofanya,” alisema Dk. Bwana.

Aidha, alisema mbegu hizo pia zinauwezo wa kukabiliana na magonjwa mbalimbali yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo wakulima wanapaswa kupewa elimu juu ya matumizi ya mbegu zilizofanyiwa utafiti na kugundulika zinastahimili changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi.

Hata hivyo, aliwataka wataalamu wa kilimo kuendelea kuwapa elimu wakulima juu ya matumizi ya mbegu bora za mazao ambazo zimefanyiwa utafiti, ili waweze kuvuna mazao bora na kuingia katika soko la ushindani.

Naye Noel Temple kutoka kituo cha kimataifa cha uboreshaji mahindi na ngano alisema wamekuwa wakifanya kazi na wakulima na wazalishaji wa mbegu za mtama, maharage na karanga.

Alisema wamekuwa wakiwasisitiza juu ya matumizi ya mbegu bora za mazao mbalimbali, ili waendeshe kilimo chenye tija.

Kutokana na hilo aliwataka wakulima hapa nchini kutumia mbegu bora za karanga zilizofanyiwa utafiti kwa ajili ya kufanya uzalishaji wenye tija utakaowainua kiuchumi wao na familia zao.

“Naomba wakulima tumieni mbegu ziluzofanyiwa utafiti na wataalam wa kilimo, lengo ni kuondokana na kilimo cha mazoea,” alisema Temple.

Alisema kuwa kulingana na utafiti waliofanya wamegundua kuwa mahitaji ya ubora wa karanga ni makubwa kwa wafanyabiashara na wasindikaji wa karanga, hivyo jitihada kubwa kwa wakulima inahitajika ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

# Wafanyakazi TANESCO watakiwa kujiwekea akiba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Gissima Nyamo-Hanga, amewaasa wafanyakazi wa shirika hilo kujiwekea akiba na kutumia fursa zinazotolewa na chama chao cha akiba na mikopo ili kujiepusha na mikopo umiza.

Nyamo-Hanga aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua Mkutano mkuu wa 56 wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo (TANESCO SACCOSS).

Alisema ni muhimu kutumia chama hicho kwa tija kwa kujiwekeza na kupata mikopo ya haraka yenye riba nafuu isiyoumiza.

“Chama hiki kilianzishwa tangu mwaka 1968 na wafanyakazi waliungana na kuamua kuanzisha ushirika huu, SACCOS hii inatoa fursa kwa wao kujiwekea akiba maana hata unapofikia muda wako wa kustaafu unakuwa na fungu lako litakalokusaidia kujikwamua kiuchumi mbali na kiinua mgongo,” alisema.

Aidha, aliwaasa wafanyakazi wa shirika hilo kujiunga kwenye chama hicho ili kupata fursa hizo, huku akiipongeza bodi ya chama hicho kwa kubuni matumizi akaunti ya mafao inayolenga kumuwekea mazingira bora ya kustaafu kwa mwanachama.

“Pia niwapongeze kwa kuendesha shughuli za chama kwa kutumia teknolojia ya kisasa yaani FOSA, matumizi ya ATM na Mobile App yanarahisisha sana huduma ndani ya chama hivyo rai yangu kwenu ni kuhamasishana na kuendelea kutumia teknolojia hii, ili kuendelea kunufaika na huduma zitolewazo na chama kwa mwanachama mmoja mmoja na chama kwa ujumla,” alisema.

**“Pia niwapongeze kwa kuendesha shughuli za chama kwa kutumia teknolojia ya kisasa yaani FOSA, matumizi ya ATM na Mobile App yanarahisisha sana huduma ndani...**

Naye Mtendaji Mkuu wa Chama hicho, Hilary Andrea, alisema wamekuwa wakitoa mikopo kwa wakati ya elimu, dharura, maendeleo isiyo na riba kubwa ili kuwasaidia wafanyakazi hao kujikwamua kiuchumi.

“Lengo letu ni kuwa na mikopo ya riba ndogo ya tarakimu moja kwenye mikopo midogo na tunatarajia kwenye mikopo mikubwa tupunguze zaidi tufikie asilimia moja au chini ya moja kwa mwaka, ili kuleta unafuu na kuwafanya wanachama wetu wasikimbilie mikopo inayoumiza kwenye taasisi zingine,” alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO SACCOS, Omary Shaban, alisema hadi kufikia mwaka 2023 chama hicho kilikuwa na wanachama 5,250 na wamekuwa wakinufaika na huduma mbalimbali za akiba na mikopo.

Alisema wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kwa jamii na kwa mwaka huu wametoa mashuka 1,750 kwa hospitali saba za mikoa na rufani.



Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Ubalozi wa Uswisi Tanzania, Holger Tausch (wa pili kushoto), akimkabidhi vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano vyenye thamani ya Sh. milioni 200, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, kwa ajili ya vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Shirika la Swisscontact, Sabine Roth na Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia Idara ya Ufundi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Dk. Erick Mgaya (kulia). **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# RC awatoa hofu wakulima wa dengu

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewatoa hofu wakulima wa dengu katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwamba tani 257,933 ambazo bado hazijauzwa kwamba zitauzwa na watalipwa fedha zao.

Akizungumza jana baada ya kutembelea ghala la kuhifadhia dengu lililoko Itigi mjini, alisema serikali itahakikisha dengu iliyoko inauzwa na kwamba kwa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi hadi sasa zimeuzwa zaidi ya tani 15,000.

“Dengu yetu kutoka Mkoa wa Singida tunauza nchini India, bahati nzuri hadi sasa sijapata malalamiko yeyote ya kwamba labda dengu yetu haina ubora hili jambo la kujivunia,” alisema.

Halima alisema changamoto ambazo zimepatikana wakati wa utekelezaji wa ununuzi wa dengu kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani zitaendelea kutatuliwa na kwamba hivi karibuni kutaitishwa kikao cha wadau kujadili namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

“Zipo changamoto za ukosefu wa maghala, vyama vya ushirika kufa, mizani na AMCOS kupitia kikao ambacho wadau ambacho tutakifanya changamoto hizi tutazojadili na kuona namna ya kuzipatia ufumbuzi,” alisema.

Awali, Ofisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Mlagazi Mgalula, alisema zao la dengu limekuwa la kwanza kwa kuingiza mapato kwenye halmashauri ambapo tangu ununuzi ulipoanza Agosti Mosi, 2024 kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani wakulima wameweza kulipwa zaidi ya Sh. bilioni 19.

Alisema hivi sasa kuna changamoto ya upatikanaji wa wanunuzi katika dengu iliyopo kwenye ghala na kwamba halmashauri imefanya mipango kutafuta wanunuzi wengine badala ya kutegemea kuuza India pekee.

Katibu wa AMCOS ya Mlowa, Emmanuel Daniel, alisema hivi sasa kuna wiki tatu bado minada haijafanyika hali ambayo imezua hofu kwa wakulima hasa ikizingatia kipindi hiki ni cha kuelekea msimu wa kilimo.

Daniel aliiomba serikali kufanya haraka kutafuta wanunuzi katika dengu iliyopo kwenye ghala, ili wakulima waweze kulipwa fedha zao na hivyo wapate nguvu kuandaa mashamba yao.





# Njombe yakabidhiwa matrekta matano

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WIZARA ya Kilimo imekabidhi matrekta matano kwa Wilaya ya Njombe, ambayo yatatumika kwenye Mradi wa Jenga Kesho iliyobora (BBT) unaotekelezwa katika halmashauri tatu za wilayani hiyo.

Akipokea matrekta hayo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema Wilaya ya Njombe ni miongoni mwa wilaya zenye mazingira rafiki ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo kutokana na hali ya hewa nzuri.

Alisema ujio wa matrekta hayo utasaidia kuwavutia vijana wengi kushiriki kwenye sekta ya kilimo kwa maelezo kuwa wengi huwa wanakwepa shughuli hizo kutokana na kukosa zana za kisasa.

Alisema matumizi ya zana hizo pia yatasaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali na hivyo kupunguza tatizo la ajira miongoni mwa vijana.

"Mwaka huu tuliamua kuanzisha BBT kwa ajili ya kuwainua wanawake na vijana, Wizara ya Kilimo imeamua kutuunga mkono kwa kutuletea matrekta pamoja na wataalamu, matumizi ya vifaa hivi yatasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija," alisema Kissa.

Alisema mbali na matrekta kutumika kwenye mradi wa BBT pia yatawasaidia wananchi wengine wa wilaya hiyo ambao watakuwa wanayakodi kwa gharama ndogo.

**Mkuu huyo wa wilaya alisema Mkoa wa Njombe ni wa tatu kitaifa kwenye matumizi ya mbolea na hivyo kuwa miongoni mwa mikoa ambayo inaongoza kwenye uzalishaji wa chakula.**

Mkuu huyo wa wilaya alisema Mkoa wa Njombe ni wa tatu kitaifa kwenye matumizi ya mbolea na hivyo kuwa miongoni mwa mikoa ambayo inaongoza kwenye uzalishaji wa chakula.

Alisema kutokana na wananchi wa mkoa huo kuwa na mwamko kwenye matumizi ya mbolea na teknolojia zingine za kilimo, pia hawatatumia nguvu kubwa kuwahamasisha kutumia matrekta hayo.

Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Agatha Mhaika, alisema serikali ya imeonyesha mwanga katika sekta ya kilimo, ili kuinua uchumi wa vijana, wanawake na makundi maalumu.

Alisema mbali na mradi huo wa BBT pia serikali inatekeleza miradi mingine kwenye sekta ya kilimo, ikiwamo ujezi wa maghala ya kuhifadhia mazao, ujenzi wa skimu za umwagiliaji pamoja na usambazaji wa mbolea ya ruzuku.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Thadei Luoga, alisema na matrekta hayo, pia serikali imetoa vipuri kwa ajili ya kufanyia matengenezo pamoja na majembe.

Alisema watatoa mafunzo kwa vijana watakaokuwa wanayatumia matrekta hayo, ili kuhakikisha wanayatumia kwa kufuata taratibu ili yadumu kwa muda mrefu.

Baadhi ya wananchi mjini Njombe, walisema zana hizo zitawasaidia kuondokana na matumizi ya jembe la mkono ambalo wamekuwa wakitumia kwa muda mrefu bila huku tija yake ikiwa ndogo.



Muuza matunda akitafuta wateja kwa madereva wa bajaji eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu wakuu wanolewa kuhusu usimamizi

**Na Gideon Mwakanosya,** RUVUMA

WALIMU wakuu 814 wa shule za msingi katika Mkoa wa Ruvuma, wamejengewa uwezo wa uongozi na usimamizi wa shule pamoja na utawala bora kwa lengo la kuboresha kiwango cha ufaulu katika mkoa huo.

Mafunzo hayo yalitolewa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), ambapo walimu hao walipatiwa mbinu mbalimbali za kuboresha sekta hiyo. Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kufunga mafunzo hayo, Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dk. Maulidi Jumanne alisema mafunzo hayo yalikuwa yanawalenga walimu wakuu wa shule za msingi za serikali pekee.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu wakuu, ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kusimamia shule husunani katika kuhakikisha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi unafanyika kwa ubora na ufanisi unaotakiwa.

"Ushiriki wa walimu hawa umekuwa ni wa asilimia 100, walimu wanastahili kupongezwa kwa mwitikio huo wa kufika kushiriki mafunzo ya uongozi na usimamizi wa shule zao," alisema Dk. Maulidi.

Awali, Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka ADEN Kituo cha Mbeya, Asha Kamando, alisema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia walimu kuimarisha uongozi na usimamizi wa shule katika mkoa huo. "Timu ya wataalamu ilishajipanga kwa kufanya maandalizi ya kutosha na imesheheni wawezeshaji mahili waliohakikisha mafunzo hayo yanaendeshwa kwa weledi, ufanisi na yanakuwa na tija kwa walimu wakuu wa shule za msingi," alisema Asha.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Ruvuma, Edith Mpinzile alisema kuwa serikali inaendelea kujitahidi kuhakikisha miundombinu ya shule za msingi na sekondari inakuwa bora.

Aliwataka walimu wa shule za msingi kutunza miundombinu ya shule na sambamba na kuipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya shule katika maeneo mbalimbali nchini.

# Viongozi wa dini wataka wanasiasa kiutunza amani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIONGOZI wa dini katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, wamewataka wanasiasa kutunza amani katika kipindi hiki cha uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuepuka kutumia lugha za chuki kwenye majukwaa.

Walitoa wito huo mwishoni mwa wiki kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Makambako kilichofanyika mjini humo.

Askofu wa Makanisa ya International Gospel Church, Abedinego Lwambale alisema neno amani limetajwa mara 226 kwenye Biblia, ikiashiria kuwa ni jambo muhimu kwenye maisha ya binadamu.

Alisema hawataraji kuona viongozi wa vyama vya siasa pamoja na wagombea wanakuwa chanzo cha kuvuruga amani kwa kutumia lugha za maudhi wanapokuwa kwenye kampeni.

"Sisi tunaendelea kutangaza amani kwamba mtu anapokwenda kupiga kura vyama vyote wazingatie kitu kinaitwa amani," alisema Askofu Lwambale.

Sheikhe wa Halmashauri ya mji wa Makambako, Ibrahimu Chang'a aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kutenda haki, ili viongozi wa kisiasa watunze amani pamoja wananchi kuchagua viongozi wanaowataka.

"Kiongozi aliyeteuliwa na chama cha siasa, wananchi utakiwa uende ukashindanishe baina ya vyama kuchagua kiongozi unayemtaka bila ya kujali kiongozi huo ni wa CCM, kiongozi huyo ni wa CHADEMA badala yake chagua atakayeweza kuongoza eneo hilo," alisema Chang'a.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya mji wa Makambako, Hanana Mfikwa aliwataka madiwani kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa haki na amani.

"Watu waelimishe umuhimu wa uchaguzi hasa wenzetu wa kanisani na msikitini tunawategemea sana kwa sababu tunawatu wengi pale twende tukawaambie haki yao na wajibu wao katika jamii kwenda kuchagua au kuchaguliwa," alisema Mfikwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Makambako, Keneth Haule alisema upo umuhimu wa kuhamasisha wananchi wote ambao walijiandikisha katika kata zote 12, mitaa 54, vijiji 14 na vitongoji 67 kwenda kupiga kura ili kuchagua viongozi wanaowataka.

Uchaguzi wa serikali za mitaa nchini kote unatarajia kufanyika ifikapo Novemba 27 mwaka huu.



## Serikali yatambua mchango mashirika ya umma

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar inatambua mchango mkubwa unaotolewa na mashirika ya umma na itaendelea kuchukua juhudi mbalimbali, ili kuhakikisha mashirika hayo yanafanya kazi kwa ufanisi mkubwa nchini.

Aliyasema hayo katika hafla ya ufungaji wa wiki ya Mashirika ya Umma Zanzibar iliyofanyika katika Kiwanja cha Mapinduzi Square Michenzani jijini Zanzibar.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa mashirika ya umma serikali imechukua hatua ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, chini ya sheria namba 6 ya mwaka 2021 na kupewa jukumu la kuwa msimamizi mkuu na mmiliki pekee wa uwekezaji wa mashirika ya umma kwa niaba ya serikali ya Zanzibar.

Makamu wa Pili alisema kuwepo kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kumechangia kuleta mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa mashirika ya umma, utoaji wa huduma kwa wananchi na kuchangia kuongezeka kwa kwa mapato ya serikali ambapo kwa mwaka 2022- 2023 mashirika ya umma yameweza kuchangia gawio la Sh. bilioni 13.7.

Hemed alisema Shirika la Bandari limeongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa meli za mizigo katika Bandari ya Malindi kupitia muwekezaji Afrikan Global Logistic (AGL) na kuchochea kuongezeka kwa mapato kutoka Sh.bilioni 5.5 hadi kufikia bilioni sita kwa mwezi kwa mwaka 2024.

Aidha, Hemed alisema kuwa Shirika la Bima la Zanzibar limepata mafanikio makubwa kwa kuendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa wananchi kwa kupitia mifumo ya TEHAMA na kuchangia kukua kwa mapato kutoka bilioni 19 kwa mwaka 2021 na kufikia bilioni 130.74 kwa mwaka 2024.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa mashirika ya umma kuendelea kuboresha mifumo ya utendaji katika utoaji wa huduma, ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu na kuendelea kukuza ushirikiano wa karibu kati ya viongozi na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kutatua changamoto mbalimbali zinapotokezea.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema kuna mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kwenye mashirika ya umma hasa katika kutoa huduma bora kwa wananchi, ili kuhakikisha yanakamilisha malengo na mikakati ya serikali iliyojiwekea.

Alisema lengo la Rais Dk. Mwinyi ni kuhakikisha kupitia Shirika la Nyumba na mashirika mengine Zanzibar inakuwa na mji wenye majengo ya kisasa yenye kukidhi huduma zote stahiki ambayo yataufanya Mji wa Zanzibar kuwa wenye haiba na muonekano mzuri utakaoitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Msajili wa Hazina Zanzibar, Wahidi Mohammed Sanya, alisema ofisi ya msajili wa hazina imefanikiwa kuyaunganisha mashirika 18 ya umma yaliyopo Zanzibar, ambayo yanafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa jambo ambalo linaifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kupiga hatua kimaendeleo kwa kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake.

Wahidi alisema wiki ya mashirika ya umma itakuwa endelevu na itafanyika kila mwaka lengo ikiwa ni kuyaweka pamoja mashirika na kujadili mafanikio, lakini pia kutafuta njia muafaka za kupata utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoyakabili mashirika hayo.

# Wawili wafariki dunia, wengine wanusurika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU wawili wamefariki dunia na wengine wawili wamejeruhiwa katika malumbano baina ya askari polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi katika Kijiji cha Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo askari walilazimika kufyatua risasi.

Tukio hilo lilitokea juzi Novemba tisa majira ya saa 12:20 asubuhi ambao waliofariki dunia ni Msina Sharif (29) na Abdalla Bakari Sheha (28) wote wakaazi wa Kidoti Mkoani humo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, kuhusu tukio hilo Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai kutoka makao makuu ya Jeshi la Polisi visiwani hapa, Zubeir Chembera alisema wakati askari polisi na askari wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama walipokuwa katika operesheni maalum mkoani humo, walikutana na watu waliokuwa na gari la mizigo likiwa halikufungwa namba za usajili aina ya Toyota Dyana.



Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jeshi la Polisi, Zubeir Chembera, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kuhusu tukio la malumbano baina ya jeshi hilo na wananchi lililotokea Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja na kusababaisha watu wawili kupoteza maisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Alisema gari hilo lilitiliwa shaka na kulisimamisha ili kufanyiwa ukaguzi na upekuzi, lakini wahusika walikataa kusimama na kuongeza mwendo na kukimbia.

Aidha, alisema askari walilikimbiza na kuendelea kukaidi kusimama, huku gari hilo likipiga honi hivyo kuhamasisha magari mengine kuingia barabarani yakiwa yamepakia watu nyuma na kuanza kushambulia kwa mawe gari hilo la polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. "Askari walifyatua risasi juu kutahadharisha kusimama pamoja na kutawanya magari yaliyokuwa yanashambulia askari hao kwa mawe, huku wakiendelea kuikimbiza gari hiyo ikiwa kwenye mwendo kasi. Lakini dereva aliendelea kukaidi hivyo gari lilipoteza mwelekeo na kugonga mti wa Mkungu, ambapo dereva wa gari na msadizi wake walipoteza maisha," alisema.

Aidha, alisema katika tukio hilo watoto wawili wamejeruhiwa ambao ni wanafunzi wa Shule ya Kidoti ambao ni Hamza Abdallah Abasi(10), Mohammed Issa Mohammed (10), ambao walikuwa wakitembea kwa miguu na kugongwa wakati gari hilo likiwa limepoteza mwelekeo na kugonga mti. Alisema majeruhi hao wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja wakiendelea kupatiwa matibabu.

Hata hivyo, alisema kufuatia tukio hilo la kusikitisha, serikali imeunda tume huru ya uchunguzi ili kufanya uchunguzi wa haraka kujua kiini cha tukio hilo, ikiwa pamoja na sababu ya gari hilo kukimbia na magari mengine kushambulia askari na askari kufyatua risasi na baada ya uchunguzi kukamilika umma utajulishwa.

"Tunaomba wananchi kuwa watulivu na tunawahakikishia kuwa taarifa kamili itatolewa mapema iwezekanavyo. Aidha tunawaasa juu ya kupokea taarifa na habari zinazosambazwa na watu pamoja na vyombo visivyo rasmi na kwamba taarifa rasmi itatolewa na tunaahidi haki itatendeka," alisema Chembera.

Awali, Chama cha ACT Wazalendo kupitia taarifa yake iliyotolewa na Hamad Mussa Yussuf, msemaji wa ofisi ya kamati ya wasemaji wa kisekta Zanzibar, alisema chama hicho kimepokea kwa huzuni tukio hilo.

"ACT tunalaani vikali mauaji haya ya kikatili na tunalitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua za haraka za kuhakikisha wanawakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria askari wao waliofanya unyama huu wa kukatisha uhai wa watu na kujeruhi wengine eti kutokana na kesi ya uchimbaji wa mchanga," alisema.

Aidha, alisema kitendo hicho hakioneshi taswira njema kwa nchi na yanatia wasiwasi na mashaka kwa wananchi juu ya utendaji na weledi kwa jeshi hilo na kuitaka serikali kulifumua kwa kulifanyia mabadiliko makubwa ya kimuundo na kuiutendaji Jeshi la Polisi Zanzibar, ili kurejesha heshima na hadhi yake ambayo ambayo tayari imepotea kwa wananchi kutokuwa na imani na utendaji.

# Balozi Uholanzi asifu uwekezaji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe De Boer, alisema mazingira ya uwekezaji Zanzibar ni mazuri kufuatia kuimarika kwa amani na utulivu wa demokrasia na kuwataka wawekezaji kutoka nchi kuwekeza katika miundombini ya huduma za mawasiliano na bandari.

Aliyasema hayo wakati alipozungumza katika mkutano wa majadiliano uliowakutanisha wawekezaji wa sekta ya usafirishaji na bandari kutoka Uholanzi pamoja na watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiongozwa na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi na Taasisi ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA).

Balozi Boer alisema katika kipindi cha miaka minne yamekuwapo mafanikio makubwa katika kuimarisha sekta ya mawasiliano na usafirishaji majini pamoja na bandari kwa kuzishirikisha sekta binafsi kufanya kazi.

Alisema ushiriki wa sekta binafsi katika kufanya kazi na kutoa huduma kwa kushirikiana na serikali ufanisi wake umeonekana, ikiwamo kuongeza kwa huduma pamoja na mapato ya serikali.

"Serikali ya Uholanzi tunaridhishwa na kazi nzuri ya mashirikiano katika utendaji wa kuleta maendeleo kwa kuzishirikisha sekta binafsi kuona zinatoa mchango mkubwa wa maendeleo ya nchi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji ZIPA, Yahya Vuai Lada, alisema mageuzi makubwa yamefanyika katika taasisi hiyo na sasa kuwa kituo maarufu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati katika uwekezaji kwa kurahisisha shughuli za uwekezaji na kuwa kituo kimoja cha kukamilisha taratibu zote "one stop centre," alisema.

"Urasimu katika mamlaka ya uwekezaji vitega uchumi ZIPA haupo tena kwa sababu tumefanya mageuzi makubwa na sasa kufikia hadhi ya kuwa kituo maarufu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki kwa wawekezaji kukamilisha usajili wa miradi yao katika kipindi kifupi sana," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari la Zanzibar, Akif Ali Khamis, alisema Uholanzi imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya Zanzibar katika sekta ya mawasiliano ambapo imetoa fedha za msaada wa ujenzi wa bandari ya Mpiga duri Zanzibar.

Aidha, alisema Shirika la Bandari la Zanzibar limefungua milango wazi na kuzishirikisha sekta binafsi za mawasiliano na katika uendeshaji wa bandari zake, ikiwamo zinazoendelea kufanyiwa ukarabati mkubwa Unguja na Pemba.

Alisema kasi ya ukarabati mkubwa wa Bandari za Wesha pamoja na Shumba Mjini unafanyika katika Kisiwa cha Pemba huku Bandari ya Wete upembuzi yakinifu ukikamilika.

"Tunazo fursa nyingi za mashirikiano katika sekta ya mawasiliano na bandari ambapo wawekezaji kutoka Uholanzi wanakaribishwa kutokana na uzoefu mkubwa wa uendeshaji katika sekta hiyo," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YAKUSAFIRIA



**RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE,** Anatangaza kupotelewa na hati yakusafiria yenye namba **TDE012463** liliyotolewa na idara ya uhamiaji 18/06/2021 Mkoa wa Dar es salaam. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/50803/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**Zahara Juma Tunda** anatangaza kupotea cheti cha Chuo kikuu chenye namba **BA (MC)0000495** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/243157/2024**

## KUPOTEA KWA BARUA YA OFA YA KIWANJA

**THECLA WANKURU KOHI**

Anatangaza katika nafasi kama msimamizi wa mirathi, Kupotea kwa barua ya ofa (letter of offer) ya shamba no **2900 na 2901.** Kilichopo chini ya jina la Yodon Mtarima Kohi, kilichopo Kisauke Mivumoni, Dar es Salaam. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi

**PHQ/DAR/KIN/244258/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**JAPHETI SAMWELI KIMARIO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 979 DEC**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa:

**PHQ/ DAR/UBU/244741/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SUZAN CLEMENCE AWANGA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **BMW 1** yenye namba za usajili **T698 EDQ**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi Taarifa:**

**PHQ/ DAR/KIN/241744/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**CHARLES MTEMI MATHIAS**

anatangaza kupotea kwa hati ya nyumba **PLOT No.32, BLOCK I CHIDACHI EAST - DODOMA CITY COUNCIL.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/50620/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MARKO JOHN PAULO**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKI PIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 280 CZJ,** MAJINA AMBAYO YAPO KWENYE KADI NI RENALDA GERLAD SILAYO AINA YA PIKIPIKI NI **BOXER BM125** RANGI NYEUSI KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/33813/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA.11605 LA MWAKA 2024**

**(Inatokana na Shauri la Maombi ya Ardhi Na.39 ya 2023 asilia shauri la Maombi ya Ardhi Na.56 la Mwaka 2016 kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Mbeya)**

**AAICO COMPANY LIMITED.................................MWOMBAJI**

**DHID YA**

**JANE JAILOS MAHALI,FURAHA MLIGO,JUMA MWANKANDE,JULIUS LUPEMBE,MWANASHILU KINYWASI NA ELISTINA KILATU.......WAJIBU MAOMBI**

**KWA: FURAHA MLIGO, POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI WA PILI.**

Unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe 21/11/2024 siku ya Alhamisi saa 03:00 kamili asubuhi bila kukosa.

**ELEWA KWAMBA**,Ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi utatolewa.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe05/11/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA.11605 LA MWAKA 2024**

**(Inatokana na Shauri la Maombi ya Ardhi Na.39 ya 2023 asilia shauri la Maombi ya Ardhi Na.56 la Mwaka 2016 kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Mbeya)**

**AAICO COMPANY LIMITED.................................MWOMBAJI**

**DHID YA**

**1.JANE JAILOS MAHALI,2.FURAHA MLIGO,3.JUMA MWANKANDE,4.JULIUS LUPEMBE,5.MWANASHILU KINYWASI, 6. ELISTINA KILATU.......WAJIBU MAOMBI**

**KWA: JULIUS LUPEMBE, POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI WA NNE.**

Unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe 21/11/2024 siku ya Alhamisi saa 03:00 kamili asubuhi bila kukosa.

**ELEWA KWAMBA,**Ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi utatolewa.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe05/11/2024.

05/11/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25182/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late AMOS RUGAKINGIRA KITEMANGANI of Kiwanja cha ndege Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ONESMO AMOS RUGAKINGIRA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 11, 2024

Date at Dodoma this 3rd Day of OCTOBER, 2024.

....................................
**PETITIONER**

**Presented for filling this 30 day of 10,2024**

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 23454/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late CHRISTINA LUSINDE SIMANDO of Chiwondo Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY EMMANUEL SIMANDO LUSINDE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of NOVEMBER, 2024

Date at Dodoma this 6TH Day of September, 2024.

....................................
**PETITIONER**

**Presented for filling this 11TH day of October,2024**

11TH ......day

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25183/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late GEORGE WAINAINA MUNGA of Nduka - Chamwino Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CELINA GEORGE WAINAINA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19 Day of 11, 2024

Date at Dodoma this 15 Day of OCTOBER, 2024

COURT SEAL DODOMA DISTRICT

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 27274 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late PROSPER MICHAEL MZERU**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANNAMARY SALES KIHEGA............... PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 10 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 11, 2024

**Dated at Dodoma this 5 Day of 11, 2024.**

....................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 226 YA MWAKA 2024**

**BAINA YA**

**ZAINABU KAISI..........................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**GEOFREY B. BADRAM..............................................MDAIWA 1**

**KWA:**
**GEOFREY B. BADRAM**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 15.01.2025 saa 3.00 asubuhi kwa ajili ya maoni ya wazee wa baraza na baadae hukumu.

**ANGALIZO:**-Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kuendelea kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07 ya Mwezi NOVEMBA, 2024.

....................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA



Rais mteule Donald Trump akifurahia jambo na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi katika hafla iliyofanyika Septemba 22, mwaka 2019 Texas. **PICHA: AP**

# Mataifa yaweka umakini kauli ya Donald Trump

## Ni kuhusu kuongezeka ushuru wa bidhaa

**Na Maulid Mmbaga**

WAKATI wa kampeni ya Rais mteule wa Marekani Donald Trump, alitishia mara kwa mara kuhusu kuongezeka kwa ushuru mkubwa wa bidhaa kutoka mataifa mbalimbali, ikiwamo asilimia 60 kwa bidhaa za China.

Beijing inachukua jukumu kubwa la umakini wake kuhusu kauli hiyo, huku India ambayo ilikuwa lengo kuu, ikiitaja nchi hiyo kama jukwaa kubwa la ushuru, akiahidi kufanya vivyo hivyo kwa malipo ya bidhaa.

Wakati Trump anajitayarisha kuchukua madaraka tena baada ya ushindi wa kushangaza dhidi ya Makamu wa Rais Kamala Harris katika uchaguzi wa rais wa Marekani, mipango yake ya vizuizi vya biashara na dhidi ya wahamiaji yanatishia kuingiza mvutano katika uhusiano wake na India.

Profesa katika Baraza la Maendeleo ya Jamii wa New Delhi, Biswajit Dhar, anasema Marekani ni kivutio kikubwa zaidi cha mauzo ya nje cha India na mara kwa mara iko kati ya washirika wake wawili wakuu wa biashara.

"Mahusiano ya India na Marekani yanaweza kuwa magumu ikiwa ahadi zote za uchaguzi ambazo Trump alitoa zitatekelezwa. Ikiwa atapitia na hii itakuwa habari mbaya sana kwa India," anasema Dhar.

Lakini anaeleza kuwa kuna matumaini mengi ya kibinafsi ya Waziri Mkuu Narendra Modi na Trump inaweza kusaidia New Delhi kuvuka barabara iliyo mbele yake.

**USHURU WA BIASHARA**

Inaelezwa kuwa biashara ya Marekani na India mwaka jana ilifikia karibu dola bilioni 120 (Sh. trilioni 321.5) na ziada ya bilioni 30 (Sh. trilioni 80) kwa India.

Pia inaelezwa kuwa biashara baina ya nchi hizo mbili imepanda kwa asilimia 92 katika muongo mmoja uliopita.

Sasa, ajenda ya Trump ya (Amerika Kwanza) ambayo inalenga kukabiliana na kupunguzwa kwa kodi ya ndani kwa kuweka ushuru wa juu kwa uagizaji inaweza kuharibu uhusiano huo.

Ingawa ushuru wa juu unaweza kuishia kupandisha gharama ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa wateja wa Marekani, inaweza pia kuumiza viwanda muhimu vinavyoelekeza mauzo ya nje ya India, kutoka teknolojia ya habari na magari hadi dawa.

Wachambuzi katika Shule ya London ya Uchumi wanatabiri hasara ya Pato la Taifa la asilimia 0.03 kwa India, na punguzo la asilimia 0.68 kwa China.

"India itakuwa miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi kwa sababu Marekani ndilo soko letu kubwa zaidi. Hicho ndicho chanzo cha wasiwasi wetu mkubwa," anasema Dhar, mtaalamu wa biashara ya kimataifa.

"Wakati wa muhula wa kwanza, Trump aliingia katika ,hali hii ya ulinzi', lakini akirudi wakati huu, atakuja akijua kwamba amepata mamlaka ya sera hizi," anasema Dhar.

Mkurugenzi wa Washington Michael Kugelman, anasema migogoro ya kimsingi ya kibiashara kati ya Marekani na India, kwasababu ya kukosekana kwa usawa katika imekaa chini ya kifuniko kwa miaka minne iliyopita chini ya utawala wa Rais Joe Biden.

Anasema mvutano unaweza kuibuka sasa na kulipuka katika utawala mpya wa Trump.

Walter Ladwig, mhadhiri mkuu wa mahusiano ya kimataifa katika Chuo cha King's, London, anakubali kwamba "biashara daima imekuwa suala gumu katika uhusiano wa nchi mbili na ilibaki mbele na katikati wakati wa miaka ya awali ya Trump".

"Tofauti na mbinu ya kutafuta marafiki wa Biden kwa vitu muhimu vya hali ya juu kama vile 'semiconductors' ni ngumu kuona Trump akiunga mkono juhudi za kuunda vitu kama hivyo popote nje ya Marekania," anasema.

**SERA YA UHAMIAJI**

Mwanadiplomasia mwandamizi wa India Anil Trigunayat, ambaye aliwahi kuwa mwakilishi wa biashara huko New York, anasema India inapojaribu kujenga uhusiano thabiti na utawala mpya wa Trump, itakabiliwa na ukweli usiowezekana.

"Marekani inajaribu kukuza watu wanaojitenga zaidi, na wakati huo huo, Delhi inajaribu kukuza ushirika zaidi ulimwenguni," anasema.

Inaelezwa kuwa kipaumbele cha kwanza cha Trump katika urais wa Marekani kiliweka alama ya wasiwasi kwa wenye visa ya H-1B, mpango wa wataalamu wa kigeni wenye ujuzi wanaotafuta kazi nchini humo.

Inaelezwa kuwa Wahindi wanawakilisha wengi wa wenye viza za aina hiyo kwa asilimia 72.3 katika mwaka uliopita. Na kwamba wafanyakazi wa China ni wa pili kwa asilimia 11.7.

Kiwango cha kunyimwa maombi ya H-1B kilipanda kutoka asilimia sita mwaka 2015 hadi 24 2018, mwaka mmoja baada ya Trump kuchukua madaraka.

Inaelezwa kuwa kiwango hicho kilongezeka zaidi hadi asilimia 30 mwaka 2020 baada ya janga la COVID-19 kuingia.

Dhar anasema mazungumzo magumu ya Trump kuhusu uhamiaji yanaweza pia kuharibu uhusiano na kwamba wakati wowote suala la uhamiaji linapopungua katika matamshi ya kisiasa, wafanyakazi wa India watahitaji kujipanga kupata athari za haraka.

Trigunayat anasema awamu ya pili ya Trump haitakuwa sawa na muhula wake wa kwanza, kwa sehemu kwasababu India sasa inajua nini cha kutarajia kutoka kwake.

"Sidhani kama uanzishwaji wa sera za kigeni za India umepofushwa na ukweli kwamba Trump pia ana vipaumbele vyake. Tutaendelea kuwa na masuala kadhaa, hasa kuhusu upatikanaji wa soko la biashara na visa vya H-1B na masuala ya uhamiaji," anasema Trigunayat.

Wataalamu wengi hata hivyo wanaamini uhusiano mkubwa kati ya Marekani na India utaendelea kukua, bila kujali ni nani aliye mamlakani.

"Modi ameanzisha uhusiano wa kibinafsi na Trump katika muongo uliopita ... huo ndio mtindo wake wa diplomasia," anasema Harsh Pant, makamu wa rais wa masomo na sera za kigeni katika Taasisi ya Utafiti ya Observer (ORF).

Vile vile, inaelezwa kuwa kurejea kwa Trump madarakani kunaweza pia kupunguza shinikizo kwa India kujiondoa katika urafiki wake wa kihistoria na Russia huku kukiwa na vita vya Moscow dhidi ya Ukraine.

Biashara ya India na Russia ilifikia kiwango cha juu mwaka huu, kiasi cha dola bilioni 65.6 (Sh. Trilioni 176) lakini hivi karibuni Marekani iliidhinisha safu ya kampuni za India kwa kusaidia juhudi za vita za Russia.

Katika hatua nyingine Trump, ameshinikiza kumalizika kwa vita nchini Ukraine, na anajulikana kupendelea diplomasia badala ya makabiliano ya kijeshi na Russia.

"Baadhi ya mivutano ambayo imekumba uhusiano wa Marekani na India katika miaka ya hivi karibuni itapungua na hiyo inajumuisha sababu ya Russia," Kugelman anasema.

Wakati huo huo, wataalamu wanasema wasiwasi juu ya jukumu la China linalozidi kujiamini katika eneo la Asia Pacific litaendelea kutumika kama gundi kati ya India na Marekani chini ya Trump.

Kadhalika inaelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, uhusiano baina ya nchi hizo mbili ulikwama kutokana na madai ya waendesha mashtaka wa Marekani kwamba maofisa wa India walijaribu kumuua mfuasi wa Sikh anayeishi Marekani.

"Trump anajionyesha kama mzalendo na kwa kuzingatia siasa zake, angeonekana kupata mafanikio ya kisiasa kutokana na kuwa hadharani kuhusu wasiwasi wake.

"Sio Russia, China, au biashara, lakini madai ya 'mauaji ya kukodisha' yamekuwa mvutano mkubwa katika uhusiano, na hii inaweza kuwa mwamko mbaya kwa India," Kugelman anasema.

# WANAWAKE ZANZIBAR WATAKIWA KUMULIKA FURSA KATIKA MICHEZO

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Nasra Juma, amesema wanawake wana nafasi kubwa ya kupiga hatua kitaifa na kimataifa kupitia sekta ya michezo mbalimbali iliyopo hapa nchini.

Amesema ushiriki wa wanawake katika michezo ni jambo muhimu na kuhamasishwa hasa katika visiwa vya Zanzibar kutokana na fursa nyingi zilizopo.

Nasra aliyasema hayo mwishoni mwa juma katika Kongamano la Wanamichezo Wanawake, lililofanyika Jumamosi katika Shule ya Tumekuja na Visiwani Zanzibar.

Kongamano hilo liliandaliwa na Kampuni ya Ving'amuzi ya Zanzibale Cable, kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWa) kwa upande wa Zanzibar na wadau wengine wakiwamo HASNET Ict Solution, Queens Travel, Abinyo Restaurant na Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar.

Alisema yeye binafsi amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupitia mchezo wa soka ambapo alikuwa mchezaji mpaka sasa kuwa kocha pekee mwanamke mwenye leseni A kwa upande wa Zanzibar, lakini kuwa Mkufunzi wa CAF.

Alisema wanawake wasidharau kwa kuona suala la michezo ni la wanaume pekee, jambo ambalo halina ukweli ndani yake.

Nasra alisema muda umefika wa kubadilisha mitazamo ya wanajamii kuhusu ushiriki wa michezo kwa wanawake hapa nchini.

Alisema ipo mifano mingi ya wanawake waliofanikiwa na kushika nyazifa za juu serikalini kupitia michezo mbalimbali ambayo waliitumikia.

"Hivi sasa dunia inawaangalia wanawake katika ushiriki wao katika michezo, hivyo tuamke tuache mitazamo ambayo haina ukweli kuwa mwanamke ni mtu wa kuangalia familia pekee. Michezo ni afya, ni ajira, lakini pia hutengeneza urafiki na watu mbalimbali," alisema.

Akifungua kongamano hilo, Msimamizi na Ofisa Mtendaji Mkuu Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki Zanzibar (COSOZA), Mtumwa Khatib Ameir, alisema wanawake lazima waamke na kuchangamkia fursa za kimichezo ndani na nje ya nchi.


Alisema mbali na michezo ni afya, lakini inasaidia kwa kiasi kikubwa kuendeleza tamaduni za nchi kupitia michezo ya kiutamadumi ambayo ipo hapa Zanzibar.

"Kuna michezo mingi ya kiutamaduni inayoweza kumtoa mwanamke kimaisha, ambayo pia inaangaliwa na kuboreshwa,"alisema.

Kwa upande wa Mratibu wa Kongamano hilo, Namal Suleiman, alisema lililenga kuwaleta pamoja wanamichezo wanawake ili kuwapa elimu na kutovunjika moyo kupitia fani zao.

Alisema Zanzibar kuna changamoto nyingi sana zinazowakabili wanawake wanaojikita katika michezo na huanzia majumbani mwao.

Kongamano hilo liliwashirikisha wachezaji soka wanawake, basketball, netaball na michezo mingine pamoja na wasanii wa maigizo, walimu wa michezo na wanafunzi.




Beki wa pembeni wa Manchester City, Rico Lewis (kulia), akijaribu kumdhibiti mshambuliaji wa Brighton, Danny Welbeck, asilete madhara langoni kwao, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Falmer juzi. Brighton ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Tabora United sasa nyodo tupu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuitwanga Yanga mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Alhamisi iliyopita, Klabu ya Tabora United imezionya timu zingine kuwa zitakutana na vipigo vikubwa zaidi kuliko ilichokipata Yanga.

Klabu hiyo imezitahadharisha timu ambazo hazijakutana nazo kwenye Ligi Kuu kujiandaa kisaikolojia, kwani baada ya ushindi dhidi ya Yanga, wachezaji wa timu hiyo wamekuwa na morali na nguvu ya kupambana kutokana na mapokezi, zawadi na pongezi walizozipata.

Wachezaji wa timu hiyo walikuwa wakipokewa kwa shangwe, kila basi la timu hiyo lilipopita kuanzia Dar es Salaam hadi Tabora baada ya ushindi huo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, amesema kama wameifunga Yanga, ina maana wanaweza kuifunga timu yoyote ile ya Ligi Kuu.

„Hizi ni salamu tosha kwa timu nyingine zote ambazo zinatakuja kucheza na sisi, baada ya mchezo dhidi ya Yanga, kama tumemfunga mbabe wa ligi, basi timu zingine zijiandae tu kisaikolojia,“ alisema Christina.

Alisema hakuna aliyeamini kama timu yao ingeifunga Yanga, lakini imefanya hivyo na lengo lao msimu huu ni kupata moja ya nafasi nne za juu ili kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

„Kila mtu alikuwa haamini kama tunaweza kuifunga Yanga, tumefanya hivyo, tumeonesha kuwa Tabora United ni timu kubwa.

„Kikosi chetu kina thamani ya Sh. bilioni mbili, kinaweza kuifunga timu yoyote, fikiria tumecheza na Yanga tukiwa ugenini, lakini tumewapiga mabao 3-1, si mara nyingi kufungwa idadi hii ya mabao.

„Tulifika siku moja kabla ya mechi, tulisafiri na uchovu wetu baada ya kucheza dhidi ya Mashujaa FC, lakini tuliweza kucheza vema na kushinda dhidi ya timu ambayo ilikuwa na siku kama nne za kupumzika baada ya kucheza dhidi ya Azam, kabla ya kucheza na sisi,“ alisema.

Alisema kikosi hicho kilitarajia kuanza mazoezi leo Jumatatu baada ya mapumziko, chini ya kocha mpya raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Anicet Kiazayidi, ambaye amekuja kuchukua nafasi ya Mkenya, Francis Kimanzi aliyetimuliwa kutokana na timu kufanya vibaya.

„Hatutokuwa na mapumziko kipindi hiki cha Kalenda ya FIFA, tuliwapa wachezaji mapumziko ya siku tatu tu, tutaendelea na mazoezi Jumatatu kwa sababu mwalimu wetu bado ni mpya,“ alisema.

## New City FC yalia na mastraika

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa New City FC, Mohamed Juma, amesema anaelekeza nguvu zake katika kufanya maboresho makubwa katika safu yake ya ushambuliaji ili kuhakikisha nafasi wanazopata wanazitumia vizuri.

New City FC juzi, Jumamosi ilijikuta ikipachikwa bao 1-0 dhidi ya Maafande wa KVZ FC katika mchezo wa kumi wa Ligi Kuu Zanzibar, uliochezwa katika Uwanja wa Mau majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza baada ya kumalizika mchezo huo, alisema timu yake hivi sasa inabadilika na inacheza vizuri kimipango.

Alisema sehemu kubwa ambayo anatakiwa kuendelea na maboresho ni safu ya ushambuliaji ili waweze kupata matokeo.

**Juma alisema nafasi nyingi za wazi zinatengenezwa, lakini wanashindwa kupachika mabao kutokana na umakini pamoja na kutokuwa na maamuzi ya haraka wanapokuwa katika lango la wapinzani wao.**

"Mchezo huu ushapita, tunaenda kuyafanyia kazi mapungufu kadhaa katika eneo la ushambuliaji na hata safu ya ulinzi ili kuhakikisha michezo mitano iliyobaki ya kukamilisha mzunguko huu wa kwanza, tunafanya vizuri," alisema.

Naye Kocha wa KVZ FC, Ali Khalid, alisema ingawa wamefanikiwa kupata alama tatu, laikini amekiri mchezo ulikuwa mgumu.

Alisema wapinzani walikuja na mipango ya ushindi kutokana na nafasi waliyoko katika msimamo wa Ligi Kuu.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na kufanikiwa kulinda bao lao walilolipata dakika za mapema za mchezo.

Kwa matokeo hayo, KVZ FC imefikisha alama 17 na kujivuta hadi nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo, wakitokea nafasi ya nane, wakati New City FC wakiendelea kubakia nafasi ya 14 na alama zake nane.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DANILLO ALENGWA

KOCHA Ruben Amorim anamlenga mlinzi wa Juventus, Danilo mwenye miaka 33, kuwa usajili wake wa kwanza Manchester United katika dirisha la Januari, kwani Mbrazili huyo anamalizia mkataba wake mwishoni mwa msimu huu. (***Mirror***)

### DIOMANDE AWANIWA

ARSENAL wanamfuatilia mlinzi wa Sporting, Ousmane Diomande mwenye miaka 20, ingawa Chelsea na Bayern Munich pia wanamtaka mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast. (***Metro***)

### RAMOS AKUMBUKWA MADRID

REAL Madrid wanafikiria kumsajili tena kwa dharura gwiji, Sergio Ramos mwenye miaka 38. (***Fichajes***)

### ARNOLD HATAKIWI BARCA

BARCELONA wameondoa nia yao ya kumnunua mlinzi wa Liverpool na Uingereza, Trent Alexander-Arnold mwenye miaka 26, ili kukidhi matakwa ya mshambuliaji wao chipukizi wa Hispania, Lamine Yamal mwenye miaka 17. (***Football365***)

### ROBERTSON MKATABA MPYA

LIVERPOOL inapania kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na beki wao wa Kimataifa wa Scotland, Andy Robertson mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### MAN CITY KIKAANGONI

KLABU za Ligi Kuu England, zimehifadhi haki ya kutafuta fidia kwa mapato yaliyopotea ikiwa Manchester City watapatikana na hatia ya kukiuka kanuni za fedha za ligi. (***Times***)

### EDU AKATAA MKATABA MPYA

MKURUGENZI wa zamani wa Michezo wa Arsenal, Edu alikataa mkataba mpya wa kubakia kwa 'Washikabunduki' hao ili kuchukua nafasi kule kwa mmiliki wa Klabu ya Nottingham Forest, Evangelos Marinakis. (***Mail***)

### BRANTHWAITE ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inapanga kumnunua beki wa Everton na England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa majira ya joto. (***Sportsport***)

### AMORIM ATAKA WA3 UNITED

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, anataka kuwasajili wachezaji watatu wa Sporting, beki wa Ureno, Goncalo Inacio mwenye miaka 23, mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande mwenye miaka 20, na mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres (26) - kuungana naye Old Trafford. (***Sacha Tavolieri***)

### MAGUIRE HAONDOKI

MLINZI wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 31, hana nia ya kuondoka Manchester United Januari na anaamini kuwa anaweza kupata mkataba mpya katika klabu hiyo. (***TBR Football***)

### DURAN AWANIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20, kutoka Aston Villa. (***Fichajes***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# GUARDIOLA, MAN CITY MAMBO MAGUMU EPL

**Tunapocheza vibaya, mimi ndiye wa kwanza kusema, sipendi lakini sina hisia...**

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anastahimili mwenendo mbaya zaidi wa takwimu katika maisha yake ya ukocha baada ya Manchester City kupoteza mchezo wao wa nne mfululizo Jumamosi.

Brighton walitoka nyuma na kuwalaza mabingwa hao watetezi mabao 2-1 katika Ligi Kuu England na kuwaacha City wanaoshika nafasi ya pili kwa pointi tano nyuma ya vinara Liverpool.

**City walikuwa hawaja poteza mechi nne mfululizo katika michuano yote tangu 2006 - miaka miwili kabla ya klabu hiyo kuchukuliwa na Abu Dhabi na miaka 10 kabla ya kuwasili kwa Guardiola.**

Kwa upande wa Guardiola, ambaye anatambulika kama kocha bora zaidi duniani, hakuwahi kupoteza mechi nne mfululizo popote katika muda wake mzuri wa uongozi ulioanza mwaka 2007.

Muda wa karibu zaidi aliokuwa nao ulikuwa msimu wa 2014-15 ambapo, pale Bayern Munich, timu yake ilipoteza kwa mikwaju ya penalti katika Kombe la Ujerumani na kufuatiwa na vipigo vitatu mfululizo - viwili kwenye Bundesliga, wakati Bayern walikuwa tayari wametwaa ubingwa, na mara moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola alipoulizwa, je, huu ni mwisho wa enzi, alijibu: „Ni nini watu wanataka, sawa? Hiyo ni kawaida - tulishinda sana. Ningependa tu kuwa na kikosi chote."

Hilo halitafanyika hivi karibuni ukizingatia kuwa kiungo nyota wa kati Rodri, mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu, atakuwa nje kwa msimu huu kutokana na jeraha.

Guardiola pia hakuwa na mabeki wake wa kati bora wanne - Ruben Dias, John Stones, Manuel Akanji na Nathan Ake, wakati mchezaji Kevin De Bruyne ni wazi hana makali au si fiti vya kutosha aliporejea kutoka chumba cha majeruhi.

"Tunapocheza vibaya, mimi ndiye wa kwanza kusema, ‚Oh, oh, siipendi.' Lakini sina hisia hizo," alisema Guardiola.

Hakika, City walikuwa na nguvu katika kipindi cha kwanza na walisonga mbele wakati Erling Haaland alipofunga bao lake la 12 la kuongoza ligi katika kampeni.

Hata hivyo, kama ilivyofungwa 4-1 na Sporting kwenye Ligi ya Mabingwa Jumanne, City hawakuweza kuendeleza kiwango chake katika kipindi cha pili na Brighton wakapambana, na Joao Pedro akisawazisha dakika ya 78 na kumtengenezea Matt O'Riley bao la ushindi dakika ya 83 katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu.

City walianza kupoteza kwa Tottenham Hotspur kwenye Kombe la Carabao wiki iliyopita, kabla ya kufungwa mabao 2-1 na Bournemouth kwenye ligi - kipigo chao cha kwanza ndani ya miezi 11.

# REAL MADRID MAJERUHI KIBAO

**MADRID,** Hispania

EDER Militao ameumia huku Rodrygo na Lucas Vazquez wakitolewa katika kipindi cha kwanza wakati wa ushindi wa mabao 4-0 wa Real Madrid dhidi ya Osasuna Jumamosi na kuzidisha majeruhi.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Militao anatarajiwa kuwa nje kwa miezi tisa, wakati Rodrygo na Vazquez wanakabiliwa na wiki tatu hadi nne nje ya uwanja.

Vinicius Junior aliifungia Madrid hat-trick na Jude Bellingham akafunga bao lake la kwanza msimu huu, lakini ushindi huo ulikumbwa na majeruhi watatu kwa Militao, Rodrygo na Vaquez.

"Ulikuwa mchezo mzuri - tuliudhibiti vema tangu mwanzo," alisema kocha Carlo Ancelotti katika mkutano wake na wanahabari baada ya mechi.

"Tangu tulipofungua ukurasa wa mabao, timu ilionekana kuwa nzuri. Majeruhi wa kipindi cha kwanza. Tunawafanyia tathmini sasa, na tutaona.

"Majeruhi watatu katika kipindi cha kwanza ni ajabu sana. Kalenda inadai sana na hairuhusu wachezaji kupumzika. Wanaenda kwenye michezo wakiwa wamechoka, hivyo hatari ya majeraha ni kubwa."

Mshambuliaji Rodrygo - ambaye alikuwa amerejea tu kwenye timu baada ya kupona tatizo la misuli ya paja - alitolewa katika dakika ya 20 pale Bernabeu na nafasi yake kuchukuliwa na Brahim Diaz.

Beki wa kati Militao alihitaji matibabu dakika 10 baadaye kabla ya kutolewa kwa machela, huku chipukizi Raul Asencio akitambulishwa badala yake.

Madrid ilithibitisha katika taarifa baadaye Jumamosi kwamba Militao amechanika nyama za misuli ya mguu wa kushoto na atafanyiwa upasuaji siku chache zijazo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alikosa mechi nyingi msimu uliopita.



MILITAO

# Liverpool yazidi kutakata EPL




**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOLl inaweza ikawa ni maamuzi ya hatima yake yenyewe katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Hiyo ni baada ya kuifunga Aston Villa kwa mabao 2-0 na hivyo kubaki kileleni kwa tofauti ya alama tano dhidi ya Man City.

Mabao ya Liverpool yalifungwa na Nunez (dk 20) pamoja na Mohamed Salah (dk 84).

Liverpool imecheza michezo 11 ya ligi mpaka sasa imeshinda michezo 9, sare moja na kufungwa mchezo mmoja.

Imefunga mabao 21 na kuruhusu sita ikiwa imekusanya alama 28, ambazo ni tano zaidi ya wapinzani wao wa karibu, Man City wenye pointi 23.

# Havertz sasa aibua matumaini Arsenal

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amepunguza wasiwasi wowote kuhusu Kai Havertz baada ya fowadi huyo wa Ujerumani kutolewa huku damu ikimwagika usoni mwake wakati wakipoteza dhidi ya Inter Jumatano.

Havertz aliongoza safu ya Arsenal katika safari yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pale San Siro, na kushindwa kuzifumania nyavu huku wageni hao wakichapwa bao 1-0.

Baada ya Hakan Calhanoglu kufunga penalti kipindi cha kwanza, Arsenal walipiga mpira mwingi na wakapiga mashuti 20 bila kukaribia kabisa kutafuta njia ya kumpita Yann Sommer wa Inter.

Wageni walikuwa bado wanasukumana katika dakika za lala salama huku Havertz akimshin- Yann Aurel Bisseck kwenye nguzo ya nyu-

Arteta aliondoa wasiwasi wowote kuhusu afya Mjerumani huyo baada ya kushindwa katikati ya juma, akifichua: „Kai, ana majeraha makubwa. Ilibidi atoke kwa sababu alihitaji kushonwa. Tunatumaini atakuwa sawa wikendi."

Havertz hakuwa mchezaji pekee wa Arsenal aliyelazimika kutolewa nje kutokana na jeraha. Mikel Merino hakuibuka kipindi cha pili baada ya kuambulia kipigo kichwani.

Kiungo huyo wa kati wa Hispania alikuwa kwenye kitovu cha maamuzi mawili ya penalti. Muda mfupi kabla ya kuadhibiwa kwa mpira wa mkono kwenye eneo la hatari la Arsenal, Merino alinyimwa mkwaju wa penalti baada ya Sommer kukosa krosi na kumpiga ngumi kichwani.

„Hapana, hakuchanganyikiwa," alisema Arteta.

Wakati Havertz na Merino wanaonekana kuepusha uharibifu wowote wa kudumu katika kupoteza,

Arteta pia aliweza kumkaribisha nahodha wake aliyemkosa sana Martin Odegaard.



## HABARI MICHEZO

### Gamondi, Yanga sasa mguu sawa

INATOKA UKURASA 24

poteza, Yanga bado iko kwenye mbio za ubingwa na ni moja kati ya timu zinazojua kuchanga karata zake kuelekea kwenye mbio hizo, hivyo kuwataka mashabiki kutokata tamaa badala yake kuendelea kuisapoti.

"Yanga ni moja kati ya timu zinazojua kuchanga karata zake kuelekea kwenye ubingwa wa Tanzania Bara kwa hiyo hii wala haitusumbui, imeshatokea imeshapita, ninachowaomba wanachama na mashabiki waendelee kuisapoti timu yao," alisema Ngai.

### Simba yapania kuanza CAF...

INATOKA UKURASA 24

zilitakiwa kucheza Novemba 21 kwa ajili ya kuzipa nafasi kujiandaa na michezo ya kimataifa.

Simba ilitakiwa kucheza dhidi ya Pamba Jiji, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Novemba 21, mchezo ambao sasa umesogezwa mbele hadi utakapotangazwa tena.

Taarifa nzuri kwa Wanasimba ni urejeo wa kiungo mkabaji Yusuph Kagoma ambaye alisema yuko katika hatua za mwisho za matibabu na wiki mbili zijazo kabla ya mchezo huo atakuwa amepona na kuanza mazoezi na wenzake tayari kwa mchezo huo.

"Kuhusu Abdulrazack Hamza yeye ameshapona na ameitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, hivyo tunakwenda kwenye mchezo dhidi ya Bravo do Maquis tukiwa kamili, itakuwa ni maamuzi kwa kocha tu ni mchezaji gani wa kumpanga na nani wa kusubiri," alisema Ahmed.

Alisema hamasa kueleka kwenye mchezo huo zitaanza Novemba 20 kuzunguka mitaani kwa ajili ya kuwaita mashabiki uwanjani.

Kabla ya mazoezi yatakayoanza leo, siku mbili zilizopita Fadlu alisema kuwa moja kati ya kazi atakazozifanya ni kuwasoma wapinzani wake ili kujua ni timu ya aina gani, inacheza vipi ili kuangalia ubora na udhaifu.

"Tutaangalia mifumo yao, jinsi wanavyocheza, ubora na udhaifu wao, ili kuwaelekeza wachezaji wetu jinsi ya kukabiliana na wapinzani wetu hasa katika mchezo huu wa kwanza ambao tutacheza nyumbani, tunataka ushindi wa kwanza na mkubwa," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

# KOCHA WA SIMBA QUEENS AAPA KULIPA KISASI KWA YANGA PRINCESS

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, amesema kikosi chake kipo kwenye maandalizi makali kwa ajili ya mchezo wa keshokutwa, Jumatano dhidi ya Yanga Princess, utakaopigwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, huku akiapa kulipiza kisasi cha kufungwa katika mechi ya Ngao ya Jamii.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Basingi kocha aliyechukua nafasi hiyo kutoka kwa Juma Mgunda, amesema hata mchezo uliopita dhidi ya Ceasiaa Queens ambao walishinda mabao 4-1, walicheza kwa uangalifu ili kutopata majeruhi ambayo yanaweza kusababisha baadhi ya wachezaji kuikosa mechi hiyo.

"Tumeshinda mchezo ule kwa mabao mengi pamoja, lakini uwanja haukuwa mzuri, hatukuweza kumiliki mpira vizuri kutokana na hali mbaya ya uwanja, nikaanza kuwatoa baadhi ya wachezaji ili wasipate majeraha kwa ajili ya kujiandaa na mchezo unaokuja," alisema kocha huyo raia wa Ghana.

Kocha huyo alisema lengo la kuwapumzisha mastaa wake ni kutaka kulipiza kisasi kwani katika mchezo huo hakuwa sehemu ya benchi la ufundi kutokana na kutokuwa na kibali yeye na baadhi ya wachezaji tegemeo wa kikosi hicho.

"Niseme kuwa mechi ya dabi haitokuwa rahisi, tuko tayari kimwili na kiakili, tumejiandaa ili kushinda kwa sababu mashabiki wetu walivunjika mioyo siku ile tulipofungwa kwenye Ngao ya Jamii, tunataka kuwafuta machozi," alisema.

Simba Queens ilifungwa kwa mikwaju ya penalti 4-3 na Yanga Princess kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii kuashiria mwanzo wa Ligi Kuu msimu huu, uliochezwa Oktoba 2, mwaka huu katika Uwanja wa KMC Complex, hatua hiyo ya matuta ilifikiwa baada ya sare ya bao 1-1.

Jumatano mchezo huo, utakuwa ni wa raundi ya nne ya Ligi Kuu, ambapo Simba Queens inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi tisa kutokana na kushinda michezo yote mitatu iliyocheza, ikifunga mabao 10 na kuruhusu mawili, ikifuatiwa na JKT Queens ambayo ina pointi saba, ikishinda mbili na sare moja, huku Yanga Princess ikiwa kwenye nafasi ya tano, ikicheza mechi tatu bila kupata ushindi wowote, ambapo imetoa sare zote na kukusanya pointi tatu.

**KWISHINE HAO...**



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Aston Villa, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi. **PICHA: MTANDAO**

# TPLB yakunwa ushindani Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Tanzania Bara (TPLB), imeeleza kufurahishwa kwake na ushindani mkali unaooneshwa na timu mbalimbali kwenye michezo yake inayoendelea.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema kwa raundi 10 ambazo timu zimecheza Ligi Kuu imekuwa na msisimuko mkali, huku ushindani ukiongezeka tofauti na msimu uliopita.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa ukilinganisha na msimu uliopita, ipo kwenye raundi ya 10, timu zingine zikiwa zimecheza mechi 11, lakini unaweza ukaona kwamba timu zote walau zimepoteza mchezo mmoja, ukilinganisha na msimu uliopita katika kipindi kama hiki kulikuwa na timu ambazo bado zilikuwa hazijapoteza mchezo," alisema Kasongo.

Alisema sababu nyingine inayoonesha ligi ya msimu huu imekuwa ngumu zaidi ni baadhi ya matokeo ya mechi kuamuliwa dakika za mwisho.

"Vile vile unaweza kuona ni jinsi gani michezo ilivyokuwa na ushindani mkubwa, tumeona michezo mingi ikiamuliwa dakika za jioni, dakika za nyongeza, kwenye sekunde za mwisho kabisa, hii inadhihirisha ushindani mkubwa," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Alisema hiki ndicho mashabiki wengi wa soka nchini na Watanzania walikuwa wakihitaji, kupata ligi ambayo ni ngumu, yenye ushindani, ambayo haitabiriki, huku akitabiri kuwa kadri inavyozidi kusonga mbele, ndivyo itakavyokuwa na ushindani zaidi kuliko huu uliopo sasa.

"Itoshe kusema kile ambacho Watanzania walikuwa wanakitarajia kupata ligi yenye ushindani sasa hivi kinaonekana, matarajio yetu ni kwamba hadi itakapofika Aprili na Mei ushindani utazidi kuwa mkali zaidi kuliko huu kwa sababu ni kipindi baadhi ya timu zitakuwa zinaelekea kwenye ubingwa, zingine kuwania nne bora kwa ajili ya kucheza mechi za kimataifa, kuna zitakazokuwa zinapambana kutocheza 'play off', na zipo ambazo zitakuwa zinapigana kutoshuka daraja," alisema.

Mpaka wakati ligi hiyo imesimama kupisha Kalenda ya FIFA, Simba inaongoza ikiwa imejikusanyia jumla ya pointi 25, Yanga iko nafasi ya pili ikiwa na pointi 24, Singida Black Stars ni ya tatu na pointi zake 23, huku Azam FC ikikamata nafasi ya nne, pointi zake 21.

Michezo

Nipashe Jumatatu Novemba 11, 2024



Guardiola, Man City mambo magumu EPL UKURASA 21

# GAMONDI, YANGA SASA MGUU SAWA

●●● Michuano Ligi ya Mabingwa yatajwa sababu huku taarifa zikizidi kueleza...



**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikidaiwa kocha raia wa Algeria, Kheireddine Madoui, kutua ndani ya Yanga, klabu hiyo imesema bado ina imani na Miguel Gamondi na inaendelea kumpa ushirikiano wa kutosha kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan, utakaochezwa Novemba 26, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Klabu hiyo, Alex Ngai, alisema juzi jioni kuwa tetesi za kwamba klabu hiyo itamtimua Gamondi na kumleta kocha mwingine hazina ukweli wowote na kuwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutokuwa na wasiwasi wowote kwani viongozi wa Yanga bado wana ushirikiano na benchi la ufundi.

"Yanazungumzwa mengi, lakini niwahakikishie wanachama, mashabiki wa Yanga kuwa viongozi wote wa Yanga wapo vizuri, tuna ushirikiano na benchi la ufundi, tutakaa na kufanya tathmini na tunaendelea na maandalizi ya mechi yetu dhidi ya Al Hilal ya Sudan, mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Black Stars tuliokuwa tucheze Novemba 21 imeshaondolewa kwenye ratiba," alisema Ngai.

Alisema pamoja na ukweli kwamba kuondolewa kwa kocha kwenye timu yoyote ile si jambo la ajabu, lakini kwa Yanga haiwezi kuwa hivi sasa kwani hakuna mpango huo kama inavyoelezwa.

"Kwa kweli siwezi kusema kama ni kweli, haina ukweli, Yanga ni timu kubwa, niwaondoe hofu tuko kwenye maandalizi, kama lolote litatokea basi haitokuwa ajabu lakini kwa sasa sitarajii kitu kama hicho.

"Tunamsapoti, tunaendelea kumpa sapoti," alisema.

Tetesi zinadai Gamondi anaweza kuondoka wakati wowote na kocha huyo kuchukua nafasi yake, huku mwenyewe akiwa amefuta utambulisho wake kama kocha wa Yanga kwenye akaunti yake katika mtandao wa instagram.

Taarifa zinasema kumekuwa na mgawanyiko kwa baadhi ya viongozi, wengine wakitaka aondoke na wengine wakitaka abaki ila kuna vitu virekebishwe na yeye mwenyewe ajirekebishe.

Akizungumzia vipigo viwili mfululizo ambavyo timu hiyo imevipata kutoka kwa Azam FC na Tabora United, Ngai alisema ni hali ya mchezo na watakaa sawa na kurekebisha mambo kabla ya kurejea tena kwenye reli.

"Sidhani kama tunapitia kipindi kigumu, ni hali tu ya mchezo, katika mpira wa miguu vitu kama hivi huwa vinatokea, bahati mbaya sana tumepoteza mechi mbili mfululizo, mfano kwenye mchezo dhidi ya Tabora, safu yetu yote ya ulinzi haikuwapo, wengine walikuwa na kadi za njano, wengine wamesimamishwa na baadhi majeruhi pia, hali ile ilituathiri sana mpaka ikafikia Khalid Aucho akarudishwa nyuma kwenda kucheza nafasi ya beki, hii ni changamoto tu tutarudi kwenye reli kama kawaida," alisema.

Katika mchezo dhidi ya Tabora United, Yanga iliwakosa Yao Kouassi ambaye ni majeruhi, Ibrahim Hamad ‚Bacca' aliyekuwa akitumikia adhabu ya kadi nyekundu na Dickson Job aliyekuwa na kadi tatu za njano.

Alisema pamoja na ku-

INAENDELEA UK. 23

## Simba yapania kuanza CAF kwa ushindi mnono

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mapumziko ya siku nne, kikosi cha Simba kinaanza rasmi leo mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa kwanza wa Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, utakaochezwa Novemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, huku ikipania kuanza na ushindi mnono nyumbani.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wachezaji watakaoanza mazoezi ni ambao hawatokwenda kwenye timu zao za taifa ambazo zinapambana kwa ajili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, zitakazofanyika nchini Morocco.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ahmed alisema baada ya mapumziko ya siku nne ambayo wachezaji wa timu hiyo waliyapata baada ya kucheza mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya KMC na kushinda mabao 4-0, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Jumatano iliyopita, wachezaji wa timu hiyo wanarejea rasmi mazoezini, Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam kujiandaa na mchezo huo chini ya kocha raia wa Afrika Kusini, Fadlu Davids.

"Kikosi kinarejea mazoezini Jumatatu baada ya siku nne za mapumziko, tukiliangalia Kombe la Shirikisho tuna uwezo wa kufanya vizuri msimu huu kwa mambo mawili. Kwanza kuanza michuano na ushindi mnono na pia tunaweza kuwa ndiyo klabu itakayokuwa inajaza mashabiki wengi zaidi kuliko zingine zinazocheza michuano hii katika michezo yote, na hili kwa mashabiki wa Simba linawezekana, deni litakalobaki ni kwa wachezaji wetu kupambana kutuletea ushindi tu," alisema Meneja Habari huyo.

Tayari Bodi ya Ligi imetangaza kuahirisha michezo ya Ligi Kuu ya Simba na Yanga ambazo

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042